# Nipashe

Jumamosi Februari 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581582

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Makonda** atishia kushtaki mawaziri kwa utendaji mbovu UKURASA 3



**Ufinyu** bajeti wakwamisha ujenzi ofisi za ubalozi UKURASA 4

**Mbaroni** kwa tuhuma wizi vifaa hospitali UKURASA 8



# Korti yatengua uamuzi wa Rais

• **NI** wa kumstaafisha utumishi DC, yaamuru arejeshwe kazini ... *Ukurasa 2*




Lori lenye namba za usajili T819 EEU, lililonusurika kuzama baada ya Daraja la Mto Ruaha kukatika katika kijiji cha Mwaya, wilayani Ulanga mkoani Morogoro mapema wiki hii. **Habari Uk. 5. PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Maeneo sita kuzinufaisha Tanzania na Poland

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na mgeni wake, Rais wa Poland, Andrzej Duda, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Bunge laibua ufisadi AICC

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA YAPELEKWA POLISI, SIMBA TRA** UK.23

**MAONI** UK.6

# Bunge laibua ufisadi mzito AICC

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeibua ufisadi wa kutisha katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) ulihusisha baadhi ya watumishi kuuza viwanja na mali huku pia likishtuka deni la Sh. bilioni 5.2 ambayo taasisi za umma zinadaiwa na taasisi hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limetoa baraka za kukamatwa, kuchunguzwa na kuchukuliwa hatua baadhi ya watumishi wanaokihujumu kituo hicho.

Aidha, imebainika kuwa baadhi ya maeneo ya kituo hicho cha diplomasia ya mikutano, ambacho hutumika kutangaza nchi kimataifa na kuvutia wageni, yamevamiwa na kujengwa miundombinu ya kudumu.

Mbali na uhujumu huo unaoathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali, ikiwamo kujenga kumbi mpya za mikutano, AICC inadai madeni makubwa kwa taasisi za umma, ikiwamo wizara mama na taasisi binafsi, yanayofikia Sh. bilioni 5.2 hadi Desemba mwaka jana.

Jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, alilieleza Bunge kuwa, AICC pamoja na mchango wake kwa uchumi wa nchi, baadhi ya watumishi wameshiriki kuuza mali za kituo, ikiwamo viwanja.

Kawawa, alikuwa akiwasilisha bungeni jijini Dodoma, taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023.

Kutokana na hujuma hizo, Bunge limeazimia hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika na wanaohusika wa kituo hicho na watakaobainika kushiriki uuzaji wa viwanja na mali za kituo kinyume na taratibu wawajibike.

Vilevile, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watu wote waliovamia na watakaovamia viwanja vya kituo hicho cha mikutano cha kimataifa cha AICC.

Wakati wa utoaji wa azimio hilo, Kawawa alisema: "Kwa kuwa vitendo vya baadhi ya watumishi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano, kuuza viwanja vya kituo hicho kinyume na taratibu vinakihujumu kituo.

"Na kwa kuwa, vitendo hivyo visipo kabiliwa kwa kuchukua hatua stahiki, dhidi ya watumishi wanaohusika na watu wengine wanovamia viwanja hivyo; hujuma dhidi ya kituo zitaendelea kukwamisha maendeleo yake na tija iliyokusudiwa na serikali.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika na wanaohusika na kituo hicho, watakaobainika kushiriki uuzaji wa viwanja na mali za kituo kinyume na taratibu; na hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watu wote waliovamia na watakaovamia viwanja vya kituo."

Akichangia mjadala kuhusu taarifa ya kamati hiyo, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega, aliitaka serikali kuzishinikiza taasisi na wizara zinazodaiwa na kituo hicho kulipa madeni yao ili kuisaidia AICC kutekeleza mipango yake ya maendeleo.

"Madeni ya takribani bilioni 5.2 ambayo wanaidai serikali, kwa nini serikali mkawape ili hiki kituo kifanye kazi, hata Wizara ya Mambo ya Nje inadaiwa. Naomba mpeleke pesa katika kituo hiki ili kifanye kazi," alisema.

Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kilichoko jijini Arusha, Kaskazini mwa Tanzania, kimekuwa sababu ya kuvutia watalii wa mikutano na matukio na hivyo kuchangia katika ukuaji wa sekta ya utalii nchini.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia), akiteta jambo na Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mahakama yatengua uamuzi Rais Samia kumstaafisha DC

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imetengua uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kumstaafisha utumishi wa umma aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Erick Kitwala.

Sambamba na kutengua uamuzi huo, mahakama imemwamuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kumrejesha katika ajira yake ya awali kabla ya kuwa mkuu wa wilaya. Pia imeamuru Kitwala kulipwa stahiki zake kwa muda wote.

Hukumu hiyo ya mahakama imetolewa jana mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu jana baada ya kumaliza kusikiliza shauri lililofunguliwa na Kitwala katika Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam, akipinga Rais kumstaafisha utumishi wa umma.

Walalamikiwa katika shauri hilo walikuwa Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akitoa uamuzi huo, Jaji Mkwizu alisema mahakama inatengua uamuzi wa Rais kwa sababu haukueleza sababu za kumstaafisha Kitwala kwa maslahi ya umma na kwamba manufaa ya umma ni suala pana.

Kitwala aliteuliwa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora Julai 27, 2018. Kabla ya uteuzi huo alikuwa ofisa sheria katika Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Juni 19, 2021 Rais Samia alitengua uteuzi wake huo wa wadhifa wa Mkuu wa Wilaya na nafasi yake ilijazwa na Dk. Yahya Nawanda.

Kutokana na uamuzi huo, Kitwala alimwandikia barua Katibu Mkuu Utumishi, akiomba amrejeshe katika ajira yake ya awali PSSF, alikokuwa akifanya kazi kabla ya kuteuliwa kuwa mkuu wa wilaya. Baada ya muda mrefu bila majibu ya barua yake, alipokea barua ya Katibu Mkuu Kiongozi ya Agosti 15, 2022 iliyomfahamisha kuwa Rais amemstaafisha kwa manufaa ya umma.

Kutokana na majibu hayo Kitwala alifungua maombi dhidi ya Katibu Mkuu Utumishi, AG na Bodi ya Wadhamini PSSSF, akiomba kibali cha kufungua shauri hili la maombi ya mapitio ya Mahakama ili kupinga uamuzi wa Rais.

Mahakama hiyo mbele ya Jaji Dk. Lilian Mongella, Mei 23, 2023 iliridhia maombi ya Kitwala na ikamruhusu kufungua shauri la kupinga uamuzi wa Rais.

Katika shauri hilo la mapitio, Kitwala aliiomba mahakama hiyo iitishe na kisha kutengua na kutupilia mbali uamuzi wa Rais akidai kuwa amekwenda nje ya mamlaka yake kisheria dhidi ya kanuni ya haki asili na ni usumbufu kwake.

Pia aliiomba mahakama imuamuru Katibu Mkuu, Utumishi amrejeshe katika ajira yake ya awali kabla ya kuteuliwa kuwa mkuu wa wilaya.

Aliiomba mahakama hiyo pia iamuru Bodi ya Wadhamini ya PSSSF kumrejesha katika nafasi yake ya awali.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
09.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumapili tarehe 11-02-2024 hadi 13-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga** kupitia **Mlandizi** gari hiyo ina namba za usajili: **T 792 DYL /T 394 DVS**

2. Gari hizo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 21.00**
   **Upana - mita 4.00**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia zitakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga** kupitia **Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
09.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumapili tarehe 11-02-2024 hadi 13.02.2024 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar- Es- Salaam Port kuelekea Mzenga, gari hizo zina namba za usajili: **T 249 EAZ / T 499 DZX, T 112 EAG / T 777 AQR**

2. Gari hiyo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 7.30**
   **Kimo - mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: Bandari ya Dar-Es-Salaam hadi Mzenga kupitia Morogoro Road

3. Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar- Es- Salaam Port** mpaka **Mlandizi Kutoka Mlandizi** kwenda **Mzenga** gari zitasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Makonda atishia kuwashtaki mawaziri

**Na Beatrice Shayo,** NJOMBE

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayeshughulikia Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, ametishia kuwashtaki kwa Rais Samia Suluhu Hassan mawaziri kutokana na kutokuwajibika.

Kutokana na hali hiyo, Makonda amewakata mawaziri kuwajibika katika majukumu yao kwa kuwa akimaliza ziara, atawasilisha ripoti kwa Rais Samia kuhusu yale aliyoyabaini.

Makonda amesema waziri yoyote akitumbuliwa itakuwa imesababishwa na kushindwa kutatua kero za wananchi, hivyo asilaumiwe Rais Samia, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango wala Waziri Mkuu Kassim Mjaliwa bali yeye (Makonda).

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Makambako mkoani Njombe katika ziara yake iliyolenga kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM na kutatua kero za wananchi.

Makonda alisema akimaliza ziara atawasilisha ripoti kwa Rais Samia Suluhu Hassan inayoonyesha kiongozi fulani hafai kwa sababu amewakuta wananchi wanateseka katika kupata huduma za kijamii.

"Nilisema jana kilichopatikana kwa maombi hakifi kwa majungu, kwa hiyo wale ambao hamfanyi kazi siku ukiona barua umebadilishwa au umetenguliwa, usimlamu Rais Samia, Makamu wa Rais, wala Waziri Mkuu bali nilaumuni mimi," alisema.

Makonda pia aliwataka mawaziri kuacha tabia ya kumsifia Rais Samia wakati wananchi wanakuwa na majonzi ya kutotatuliwa kero zao.

Kadhalika, alimwagiza Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji na Naibu wake, Exaud Kigahe, kutojifungia ofisini bali wafanye ziara ya kutatua kero za wafanyabiashara.

"Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu wake wafanye ziara. Juzi nilisema ninyi wateule mkifanya kazi yenu Makonda, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, Makamu Mwenyekiti wa Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana na Katibu wa Oganizesheni, Issa Gavu, kazi yetu inakuwa nyepesi sana," alisema.

Makonda alisema wafanyabiashara wengi wanaichangia CCM si kwa sababu wanakipenda bali wana hofu kwa sababu wasipotoa wanadhani wanaweza kuletewa ofisa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo wanajikuta ni miongoni mwa waathirika kwa sababu hawajachangia chama.

"Ninatumia hadhara hii kumtaka Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara aonekane akizunguka nchi nzima akisikiliza kero za wafanyabiashara na kuzitafutia majibu," alisema Makonda.

Alisema wafanyabiashara hao wana matatizo na kwamba Rais Samia ameshateua watu na kuwapa sekta ya kushughulikia na kutafuta majibu yao.

"Tunakopita tunaona wafanyabiashara wanalia wakionyesha matatizo ambayo kama tutawasikiliza hakika watakuwa sehemu ya kuijenga nchi yao na wao kunufaika na fursa zilizopo ndani ya nchi yao.

"Fanyeni ziara zenu. Nimefurahi leo nilikuwa naangalia video moja nikamuona Waziri wa Maji, Jumaa Aweso anamhoji bosi wa maji ambaye amechukua Sh. milioni 600 za ujenzi wa bwawa la maji, anamwambia twende katika bwawa wamefika anamhoji bwawa lipo wapi tuonyeshe halionekani, akamuuliza, wewe si umechukua hela na ukalipwa? Anajibu ndiyo! bwawa liko wapi? halipo," alisema Makonda.

Alisema kama Waziri Aweso angebaki ofisi asingejua kama Sh. milioni 600 hazijachimba bwawa, angesoma kwenye taarifa na kuona mambo yote yapo sawa.

# Maeneo sita kuzinufaisha Tanzania, Poland

**Na Restuta James**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Poland, Andrzej Duda, wamekubaliana kuimarisha uhusiano katika nyanja tano na sekta sita za kimkakati.

Wakuu hao wa nchi walitangaza makubaliano hayo Ikulu jijini Dar es Salaam jana, walipozungumza na waandishi wa habari, ikiwa ni sehemu ya ziara ya Rais Duda nchini.

Akizungumza katika mkutano huo, Rais Samia alisema ziara ya Rais Duda ni ushahidi wa kuendelea kuimarika kwa uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizo mbili ambao umekuwapo kwa miaka 62 sasa.

"Ziara inatupa fursa ya kuimarisha uhusiano wetu wa kiuchumi na Poland ambayo ina uchumi wa 21 kwa ukubwa duniani, tumekuwa na mazungumzo mazuri kuhusu maeneo ya kushirikiana katika nyanja za elimu, kilimo, biashara, uwekezaji na utalii.

"Tumekubaliana pia kwenye maeneo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), tumekubaliana kuendelea kuimarisha uhusiano uliopo na kuhamasisha uwekezaji zaidi kwenye sekta za kimkakati kama vile viwanda, uzalishaji, nishati, madini, gesi asilia na uchumi wa buluu," alisema.

Rais Samia alisema Poland ni moja ya wabia wakubwa wa Tanzania kutoka Umoja wa Ulaya na kwamba ni miongoni mwa nchi 10 ambazo raia wake wengi wanafika nchini kutalii.

Kwa mujibu wa Rais Samia, takwimu za mwaka mmoja uliopita zinaonyesha kwamba watalii 41,000 kutoka Poland walitembelea Tanzania na ndani ya mwezi mmoja wameshawasili 6,000.

"Tumewaelekeza wataalamu kuandaa safari za ndege za moja kwa moja toka Tanzania kwenda Poland na tumeweka ombi hilo kwa msisitizo sana kwa wenzetu," alisema.

Pia alisema Poland imekuwa ikichangia shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye sekta ya afya na kwamba ziara ya Rais Duda itaimarisha miradi ya utoaji huduma katika hospitali tano nchini.

Alizitaja hospitali hizo kuwa ni Aga Khan, Kituo cha Afya Chanika, hospitali za rufani ya mikoa za Temeke na Mwananyamala pamoja na za Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza.

Samia alimshukuru kwa utayari wa nchi yake kupitia wakala wa mikopo ya usafirishaji nchini humo, kutoa bima kwa benki za biashara nchini kwa ajili ya kutekeleza mradi wa reli ya kisasa vipande vya Makutupora hadi Tabora na Tabora hadi Isaka.

"Kwa utayari huo inadhihirisha Poland inatambua umuhimu wa mradi huu kwa Tanzania katika kukuza biashara katika nchi za Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla. Wataalamu wetu wanaendelea kukamilisha taratibu zitakazowezesha wabia wetu Poland kushiriki mradi huu," alisema Dk. Samia.

Alisema kwenye utalii, biashara na uwekezaji, Tanzania imewakaribisha Wapoland kuwekeza hasa kwenye ujenzi wa hoteli za kitalii.

Kadhalika, Rais Samia alipokea mwaliko wa Rais Duda aliyemkaribisha Poland kwa ziara ya kiserikali.

Kuhusu mradi wa matrekta na ujenzi wa vihenge unaofadhiliwa na serikali ya Poland, Rais Samia alisema bado haujakamilika na timu za wataalamu zimeelekezwa kujadiliana na kuona namna ya kuukamilisha.

Katika hatua nyingine, Rais Samia alisema timu ya wataalamu imeshaelekezwa kuchukua hatua zitakazowezesha kuanza kwa safari za moja kwa moja kati ya Poland na Tanzania.

Alisema safari hizo zitachochea zaidi utalii pamoja na biashara kwa kuwa Poland ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kuwa na watalii wengi nchini.

**RAIS DUDA**

Rais Duda ambaye aliambatana na mawaziri waandamizi na wafanyabiashara, alisema Poland ina utaalamu mkubwa kwenye uzalishaji viwandani, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kuunda mifumo madhubuti ya kibenki na udhibiti wa makosa ya mtandao.

Alisema kwa Ulaya, kampuni za Kipoland ni kiongozi katika TEHAMA na kwamba watafadhili vijana wa Tanzania kwenda kusoma Poland katika eneo la udaktari, kilimo, madini, utafiti na maeneo mengine ambayo yatainufaisha Tanzania watakapohitimu.

Alisema moja ya kampuni za nchi hiyo inayozalisha taa zinazotunza mazingira (Green tech), imeonesha nia ya kufungua tawi lake hapa nchini. Pa alisema wamekubaliana na kuzielekeza timu za wataalamu zikae na kuainisha maeneo ya kushirikiana kibiashara.

"Tumekuwa na uhusiano wa kidiplomasia kwa zaidi ya miaka 60. Tanzania ilipokea wakimbizi zaidi ya 5,000 kutoka Poland wakati wa vita vya pili vya dunia. Nimeongea na Rais namna ya kutanua mipaka ya ushirikiano wetu kibiashara," alisema Rais Duda.

Alifafanua kuwa raia wa nchi yake wataendelea kuja Tanzania kutalii, kwa sababu uchumi wao umeimarika na watu wameanza kutumia fedha zao kuliko ilivyokuwa mwaka jana.


## TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku saba (7) na siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MANASA OMARY MANDITI | GABRIEL GAUDENCE MGUNDA | RESIDENTIAL LICENCE NO KND028511, ARDHI Na. KND/KWE/KUK11/51 | UKWAMANI, KAWE MANISPAA YA KINONDONI | Tarehe 19/02/2024 na kuendelea, saa 4:00 asubuhi na kuendelea | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | JOYCE G. MWASABWITE | GWALUGANO OBASI MWASABWITE | CERTIFICATE OF OCCUPANCY NO 34098 BLOCK G MBAGALA AREA | MBAGALA, MANISPAA YA TEMEKE | Tarehe 04/03/2024 na kuendelea, saa 4:00 asubuhi na kuendelea | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada ata lazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasilianana:**

LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD
P.O.Box 68172
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559
Email: lehalelglc@gmail.com

# Ukata wakwamisha ujenzi ofisi ubalozi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

LICHA ya serikali kupewa miezi 12 kuviendeleza viwanja vya Ubalozi vya Addis Ababa (Ethiopia) na Abuja (Nigeria) ili kuepuka kupoteza umiliki wake kwa kutwaliwa na mamlaka za ardhi za nchi hizo, Bunge limesema hadi kufikia Januari, mwaka huu, miradi hiyo imekwama kuanza kutokana na ufinyu wa bajeti.

Viwanja hivyo, vimepangwa kuendelezwa kupitia Mpango wa Ujenzi wa Ofisi za Balozi na Majengo ya Kitegauchumi, kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inatekeleza mkakati mahsusi wa miaka 15 (2017/18 - 2031/32) wa uendelezaji wa viwanja na majengo ya serikali balozini.

Mkakati huo unalenga kuboresha mazingira ya utekelezaji wa majukumu ya watumishi ubalozini, kutunza na kuimarisha taswira njema ya taifa nje ya nchi pamoja na kutumia majengo hayo kama vitegauchumi kwa madhumuni ya kuongeza wigo wa mapato ya serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, akiwasilisha jana bungeni jijini Dodoma taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023, alisema viwanja vya Addis Ababa, serikali ilipewa miezi tisa, tangu Februari mwaka jana, kuviendeleza.

Aidha katika kiwanja cha Abuja, alisema serikali ilipewa miezi mitatu tangu Oktoba, mwaka jana, lakini hadi kufikia Januari, mwaka huu, utekelezaji wa miradi hiyo ulikuwa haujaanza.

Wizara hiyo, ina miradi 36 itakayotekelezwa katika kipindi cha kuishia mwaka 2031/32.

Kati ya miradi hiyo, 16 ni ya kipaumbele na wizara hiyo imeanza utekelezaji wa miradi sita, ambayo ni Nairobi (Kenya), Kinshasa (DRC), Addis Ababa (Ethiopia), Kampala (Uganda), Abuja (Nigeria) na Lusaka (Zambia), ambayo wabia wameonyesha nia ya kushiriki katika utekelezaji.

Kutokana na jambo hilo litakalokwamisha kufanikiwa kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Ubalozi wa Tanzania, Bunge limeazimia, bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania, yakiwamo majengo ya vitega uchumi, itengwe kulingana na mahitaji ya miradi ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania.

Kadhalika, bajeti inayotengwa na kupitishwa na Bunge, kwa ajili ya miradi ya ujenzi katika Balozi za Tanzania, ipatikane kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya ujenzi ya majengo na vitega uchumi katika Balozi za Tanzania.

Kuhusu hatari ya viwanja vya ubalozi kutwaliwa, Kawawa, ambaye ni Mbunge wa Namtumbo (CCM) alisema: "Kwa kuwa kutokuendeleza viwanja vya Ubalozi wa Tanzania uliopo Addis Ababa na Abuja, kulisababisha mamlaka za nchi zinazohusika kutoa muda maalumu kwa Tanzania kuwa imeendeleza viwanja hiyo.

"Na kwa kuwa kutokuendelezwa kwa viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa kutasababisha kutwaliwa kwa viwanja hivyo; jambo ambalo litaharibu sifa na kuvuruga hadhi ya nchi yetu kwenye medani za kidiplomasia.

"Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, zipange upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya kuendeleza viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa."

Akichangia mjadala kuhusu mpango huo, Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, alisema mpango huo umekuwa ukikumbwa na tatizo kubwa la kibajeti.

"Mpaka leo tunavyozungumza, mpango huu wa miaka 15, miaka mitano sasa umekuwa unasuasua na utekelezaji wake umekuwa ni wa shida sana. Lakini moja kati ya changamoto zilizopelekea mpango huu kutotekelezeka kwa muda uliopangwa ni bajeti.

"Sasa pamoja na tatizo hilo la kibajeti pamoja na wizara kuanza kufikiri kuingia kwenye makubaliano na sekta za umma na sekta binafsi ili kuweza kushirikiana kufanya maboresho kwenye majengo yetu na Balozi zetu kule nje, lakini shida kubwa vilevile imekuwa ni muda unaochukuliwa kwa ajili ya kufanya majadiliano na taasisi hizi," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida, Kemirembe Lwota (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jimson Mhagama (katikati), alipotembelea kukagua ujenzi wa bwalo la Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Solya, wilayani humo juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanaotibu 'red eyes' kienyeji waonywa

**Na Christina Mwakangale**

WIZARA ya Afya imetoa tahadhari kwa umma kuhusu ugonjwa wa macho mekundu maarufu kama 'red eyes', kutokana na kukithiri kwa idadi ya wanaougua, wengi wakitumia tiba bila kufuata ushauri wa daktari.

Imesema tangu kutokea kwa ugonjwa huo watu wanne wamegunduliwa kuwa na dalili za upofu kulikosababishwa na matumizi ya dawa za asili katika matibabu.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, huku akibainisha kuwa Januari 16, mwaka huu, wizara ilitoa taarifa ya kuwapo kwa ugonjwa huo nchini ingawa wamegundua baadhi ya watu wanatumia dawa bila ushauri.

Alisema mikoa inayoongoza kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa ni Dar es Salaam na Pwani, huku akiwaomba viongozi wa dini kuhimiza waumini kuacha kupeana salamu kwa mikono ili kupunguza maambukizi.

Kadhalika alisema hadi Februari 3, mwaka huu, ugonjwa huo umeshaenea katika mikoa 23 pamoja na nchi jirani, umesababisha zaidi ya watu 12,332 kuugua hapa nchini.

"Tunatoa tahadhari na kutoa msisitizo hao ni idadi ya waliofika katika vituo vyetu, wengine hawajaja kutibiwa. Ugonjwa hupona wenyewe. Mwili utajitengenezea tiba wenyewe. Tangu kuugua na kupona huchukua muda wa wiki mbili hadi sita," alisema Prof. Ruggajo.

Alisema ugonjwa huo unaambukizwa kwa kugusa machozi au tongotongo ama vitasa, kalamu, kuchangia taulo, leso, mashuka, kwamba hauambukizwi kwa njia ya hewa wala kumwangalia mgonjwa.

"Tumeanza kupokea taarifa kwamba kuna wagonjwa wakiwa tayari wana vidonda katika mboni ya jicho. Wengi wanafuata tiba katika mitandao ya kijamii, dawa zisizo rasmi kama vitakasa mikono, chai yenye majani ya chai mengi, tangawizi, maji ya chumvi, maziwa ya mama na hata mikojo ya binadamu," alisema.

Alisema wanaougua ugonjwa huo wanapaswa kunawa uso kwa majisafi, pia wasinunue dawa kiholela na kwamba wapate huduma za dawa kwenye maduka, waache kutoa dawa bila kutumia taarifa kutoka kwa daktari.

Alisema: "Hatua kali zitachukuliwa ikiwamo kuwafutia leseni wanaotumia dawa bila ushauri wa daktari. Si kila macho mekundu ni 'red eyes'. Tuzuie kugusa macho inavyowezekana, tusishikane mikono. Sehemu za ibada wapo wanalazimishwa kushikana mikono. Wapeane amani kwa kuinamana," alieleza Prof. Ruggajo.

# Waziri ahimiza upendo kuleta ufanisi utendaji

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amesisitiza upendo miongoni mwa watumishi ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Pia amewataka watumishi hao wa sekta ya ardhi kufanya kazi kwa bidii ili serikali ione matunda na ufanisi wa kazi walizotumwa kuzitekeleza.

Pinda alisema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na viongozi na watumishi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, makao makuu.

Alisema akiwa Naibu Waziri, asingependa watumishi wa sekta hiyo kuishi bila upendo ndiyo maana ameamua kukutana na kada zote za watumishi kwa lengo la kujua changamoto za watumishi wa kada hizo.

Kwa mujibu wa Pinda upendo miongoni mwa watumishi si tu unatoa faraja bali unarahisisha kazi za wizara kwa kuwa watumishi hao watakuwa wakifanya kazi kwa furaha na amani.

Alibainisha kuwa uamuzi wa kukutana na watumishi unalenga pia kuwafunda na kuwaweka karibu watumishi ili Wizara ya Ardhi ifanye kazi kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya.

"Nimeona nikae na watumishi kwa hekima na busara ili nifahamu changamoto zinazowakabili na kuzitatua ili mwisho wa siku kuondoa malalamiko yanayotolewa kwa wizara," alisema na kuongeza kuwa:.

"Shati letu limejaa madoa, ukipita mtaani wakiona mtumishi wa ardhi wanasema ni wale wale na sauti za kulaumu ni kali kweli kweli."

Pinda pia aliwataka watumishi wa sekta hiyo kupewa stahiki zao kwa mujibu wa sheña, taratibu na miongozo iliyopo ili wafanye kazi kwa bidii bila manung'uniko.

"Watumishi wakipewa posho stahiki utaona jinsi wanavyokimbiza mambo na ugumu utaisha," alisema.

## EALA yakoshwa na utendaji TPA

**Na Mary Geofrey**

WABUNGE wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), wameipongeza Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa kutekeleza vyema majukumu ya kuhudumia shehena kubwa za mizigo na kusaidia kufungua korido ya Afrika Mashariki.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji ya EALA, Rutazana Francine, baada ya kukamilisha ziara iliyolenga kujifunza utendaji kazi wa Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wana kitu cha kujifunza kwa Tanzania kupitia bandari hiyo yenye uwezo mkubwa wa kushusha kontena nyingi za mizigo kwa muda usiozidi siku tano.

"Tupo Tanzania kwa ziara yetu ya kikazi hapa bandarini, tumefanikiwa kutembelea maeneo kadhaa na kujionea namna shughuli hapa zinavyoendeshwa kwa saa 24, tumeridhishwa sana na nichukue fursa hii kuipongeza serikali ya Tanzania kwa uwekezaji huu mkubwa," alisema Rutazana ambaye ni mwakilishi wa bunge hilo kutokea Rwanda.

Naye mjumbe wa bunge hilo kutoka Kenya, David Ole Sankok, alisema walifika bandarini hapo kujifunza namna Afrika Mashariki inavyonufaika na korido na wameridhishwa na jitihada zinazofanywa na TPA.

Alisema wamebaini Tanzania ina uwezo wa kupokea kontena nyingi za mafuta zinazoweza kupakuliwa na kusambazwa katika nchi zote za Afrika Mashariki. Aidha alisema Tanzania ina nafasi ya kupiga hatua kubwa ya mafanikio kupitia uchumi wa buluu kutokana na kumiliki eneo kubwa la bahari.

Sankok alisema wamesikia matatizo ya wafanyabiashara wanaotumia bandari ikiwamo ucheleweshwaji wa mizigo, hivyo watatengeneza sheria ambazo zitawasaidia kufanya biashara zao kwa ubora zaidi.

Naye Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mussa Biboze, alisema wabunge hao wamejifunza mengi kupitia ziara hiyo, kwamba jukumu la TPA ni kuendelea kuongeza ufanisi kila siku.

Alisema kuna matatizo machache ambayo wanazifanyia kazi ili kurahisisha utendaji kazi wa bandari hiyo.

Biboze alisema mizigo ya ndani inapofika bandarini hupakuliwa ndani ya siku tano na ile ya nje ya nchi wana mikataba ya siku 24 hadi 30.

# Maofisa ardhi wakalia kuti kavu

**Na Beatrice Shayo,** IRINGA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amewaagiza maofisa ardhi wanne wa Manispaa ya Iringa kufungasha virago, baada ya kutajwa na wananchi kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi mkoani hapa.

Alitoa maagizo hayo jana katika mkutano uliofanyika viwanja vya Mwembetogwa mkoani hapa uliolenga kusikiliza kero za wananchi.

Wakati wa mkutano huo, kila mwananchi aliyepewa kipaza sauti ili awasilishe kero yake alizungumzia migogoro ya ardhi huku wakiwataja maofisa ardhi hao kuhusika katika kuwanyima haki zao.

Mmoja wa maofisa hao ni Mthamini Ardhi wa Mkoa wa Iringa, Priscus Shirima, ambaye ametajwa kuwa kinara katika migogoro hiyo ya ardhi, mmoja wa wananchi alieleza kuwa aliombwa Sh. milioni tatu kwa ajili ya kutoa mchoro wa nyumba, kwamba mpaka sasa ni miaka minne imepita hajapewa huo mchoro.

"Kwenye simu yangu ina meseji 39,000 na kila mmoja ukiisoma ni matatizo. Kuna wakati mwingine nashindwa kuvumilia najikuta nalia, vingine ukisimuliwa huna uwezo wa kuvibeba mnavyonyoosha mikono najisikia vibaya kwa sababu sina uwezo wa kuwasikiliza wote," alisema Makonda.

Kutokana na kukithiri kwa malalamiko ya migogoro ya ardhi katika mkutano huo, Makonda alilazimika kuwaita maofisa wa ardhi na kuwauliza wana miaka mingapi kazini, ambapo kila mmoja alijibu kulingana na muda wake kazini, huku wengine wakisema wana miaka mitatu, 10, sita, 13

"Wewe uliyesema una miaka 10 na wewe wa miaka 13 mjiandae kuhama. Nilitaka muone huwezi kuwa na ofisa ardhi unakaa eneo moja zaidi ya miaka 13 halafu ukategemea kutakuwa na usawa, kesho (leo) mnavyonikabidhi nyaraka ya hawa wananchi nitaongea na mabosi wenu lazima yafanyike mabadiliko," alisema.

"Lakini si tu hivyo na wote wenye miaka minne na kuendelea mliokaa sehemu moja lazima wachunguzwe utendaji wao wa kazi ili unapohamishwa tusihamishe tatizo inawezekana umeharibu hapa umezalisha migogoro tukakupeleka sehemu nyingine ukaenda kuendeleza tabia hiyo. Ndugu zangu maofisa ardhi wenye miaka miaka 10 hadi 13 mjiandae," aliongeza.

Makonda alisema mtendaji anapokaa muda mrefu katika kituo kimoja huenda akawa ni mtendaji mzuri au ana mtandao wa kula rushwa na viongozi wakubwa ambao wanamwacha.



Meneja wa Bandari ya Mtwara, Ferdinand Nyati (wa pili kulia), akiwaeleza wahariri kuhusu maboresho ambayo yamefanywa na bandari hiyo, walipotembelea mkoani Mtwara jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wavuka mto kwa mtumbwi baada ya daraja kukatika

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKAZI wa Kata za Ilonga, Ketaketa, Mwaya na Mbunga katika wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro wanalazimika kuvuka Mto Ruaha kwa kutumia mtumbwi wa asili kwa gharama ya Sh. 1,000.

Hali hiyo inatokana na kukatika kwa daraja la mto huo kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Wakizungumza katika eneo la tukio lilipokatika daraja hilo juzi, mmoja wa wakazi wa kijiji cha Mwaya katika daraja hilo, Michael Likomawagi, alisema wananchi wa vijiji hivyo, ambao wengi ni wakulima na wafanyabiashara, wanapata adha, hivyo yeye kulazimika kuwasaidia kuvuka kwa kutumia gome la mti.

Diwani wa Mwaya, Edson Williamson, alisema daraja hilo lilikatika wakati ujenzi wa barabara ukiendelea katika eneo hilo baada ya kuharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Kutokana na hali hiyo, Mbunge wa Ulanga (CCM), Salim Hasham, alisema katika kukabiliana na adha ya usafiri kwenye daraja hilo, tayari wameshachanga Sh. milioni 2.7 na kufanya ujenzi wa kivuko cha muda kabla ya daraja kamili kukamilika.

Naye Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Patrick Rambika, alisema daraja hilo lilikatika Februari 5, mwaka huu na sasa mkandarasi yuko eneo la tukio kuhakikisha eneo hilo linapitika.

Mhandisi Rambika alisema daraja hilo lilikuwa la chuma na tayari vyuma vya kulirejesha katika hali yake vimeshafika eneo la tukio na mafundi wanaendelea kufunga ili njia hiyo iendelee kupitika.

Alisema kwa sasa kuna njia ya kupita kwa miguu na mitumbwi pekee lakini usafiri wa vyombo vya moto bado haujaanza kutokana na ukubwa na upana wa mto huo.

Aidha, Mhandisi Rambika alisema katika Mkoa wa Morogoro kuna maeneo mengi yaliyoathirika na mvua inayoendelea kunyesha na mengi yamesharudishwa na yameshaanza kupitika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji maandalizi ya AFCON 2025 mapema

**FAINALI** za Mataifa ya Afrika 2023 zinafika ukingoni kesho Jumapili nchini Ivory Coast ambapo wenyeji watamumana na Nigeria katika mchezo unaotazamiwa kuwa wa ushindani mkubwa.

Fainali hizi zinamalizika huku Ukanda wa Afrika Mashariki katika Baraza la Soka (CECAFA) timu ya pekee iliyoshiriki ni Tanzania tu ambayo hata hivyo iliishia hatua ya makundi.

Taifa Stars imecheza michezo mitatu kwenye kundi lake la F wakiwa na timu za Morocco, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Zambia ambapo kwenye kundi hilo Stars ilipoteza mchezo mmoja tu baada ya kufungwa na Morocco mabao 3-0.

Michezo iliyobakia Taifa Stars ilitoka sare na Zambia 1-1 na Congo 0-0 na kuhitimisha ushiriki wao kwa fainali za mwaka huu.

Kumalizika kwa fainali hizi ambazo zimekuwa na msisimko mkubwa ni mwanzo wa fainali zijazo za mwaka 2025 ambapo kampeni zake zitaanza hivi karibuni, nchi Mwanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) zitaanza kampeni ya kusaka tiketi.

Katika nchi hizo ipo pia Tanzania ambayo itatafuta nafasi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya nne kabla ya kugeukia zile za mwaka 2027 ambapo itakuwa moja ya nchi mwenyeji.

Ni wazi Taifa Stars kipo ilichojifunza kwenye fainali zinazomalizika kesho na hivyo watakuwa na nafasi ya kurekebisha au kuongeza katika maeneo ambayo wanaona yaliwaangusha kwenye fainali za mwaka huu.

Si tu kwa kikosi cha Taifa Stars, lakini kwa viongozi wa mpira wetu, tunamaanisha Shirikisho la Soka Tanzania na serikali kwa ujumla watakuwa wameona nini kifanyike kuelekea kwenye fainali zijazo ili Taifa Stars ifanye vizuri.

Nipashe tunaamini maandalizi ya mapema ni moja na njia ya kufanya vizuri kwenye mashindano yajayo ya AFCON.

Maandalizi ya timu yetu kuelekea michezo ya kutafuta tiketi ya kushiriki fainali za Afrika yaanze mapema kwa kuandaa timu itakayotuhakikishia tiketi ya ushiriki wetu kwa mara ya nne.

Tunaamini kushiriki fainali za 2025 kutatusaidia kwa kujenga timu yetu kuelekea fainali za 2027 ambazo Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda tutakuwa wenyeji wa michuano hiyo.

Kufanya vizuri kwenye soka hakuji kama upepo, ni maandalizi na mikakati mizuri kuanzia ngazi ya taifa kwa maana serikali, Shirikisho la Soka na timu yenyewe kwa ujumla wake.

Kwa mara ya pili Taifa Stars imeishia hatua ya makundi, tunaamini mara hizo zinatosha kuipa nafasi timu yetu kujifunza namna ya kufuzu kwenda hatua ya 16 bora na baadaye robo fainali na kuendelea.

Timu ambazo hazikupewa nafasi ya kufanya vizuri AFCON ya mwaka huu kama Namibia, Guinea au mali zote zimeweza kufanya vizuri kutokana na maandalizi na mipango mizuri waliyoiweka miaka ya nyuma.

Taifa Stars inaweza kufanya vizuri kwenye fainali zijazo kama tu mikakati mizuri itawekwa, kuwa na benchi zuri la ufundi lenye makocha wenye uwezo na kufanya uchaguzi sahihi wa wachezaji.

Mashabiki na wadau wa soka hapa nchini, tunasubiri kwa amu fainali zijazo za AFCON tukiamini kwa mara nyingine, 2025 Taifa Stars itashiriki na kuiwakilisha tena Afrika Mashariki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Bodi isiruhusu mechi za ligi ziwe kama za 'uswahilini'

**VITUKO** kama hivi niliviona zamani sana wakati huo kipa akiwa Ivo Mapunda. Wakati akitoka Gor Mahia na kujiunga na klabu ya Simba alikuwa na taulo lake lenye ukubwa zaidi ya taulo la kawaida la kipa analotumia kujifutia jasho uwanjani.

Kutokana na hilo, waamuzi walikuwa hawaruhusu aling'inize kwenye nyavu kwani ingeweza kusababisha kupanua zaidi nyavu na mpira ungeweza kupenya na kuleta utata.

Akawa analazimishwa kuliweka kando ya lango na alifanya hivyo. Lakini baadhi ya mashabiki hawakuamini kama ni taulo la kawaida, wakawa wanaruka uzio na kwenda kulipora na kukimbia nalo.

Hilo lilikuwa jambo la kawaida kutokea zaidi ya miaka 10 iliyopita wakati ligi yetu ilikuwa bado haijapiga hatua kubwa sana.

Kwa sasa Ligi ya Tanzania ni moja kati ya ligi yenye heshima kubwa Afrika, inashika nafasi ya sita sasa.

Mwaka huu imetoa wachezaji 19 kwenda kucheza michuano ya AFCON wakiwa kwenye timu tano tofauti, ambazo ni Taifa Stars, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, Mali na Zambia.

Wachezaji wa timu wanaocheza Ligi ya Tanzania walizisaidia timu zao kutinga hadi hatua za robo fainali na nusu fainali.

Golikipa wa Yanga, Djigui Diarra aliyeichezea Mali na kiungo wa timu hiyo, Stephane Aziz Ki, akiwa na timu yake ya taifa ya Burkina Faso, walikutana hatua ya 16 bora, na Diarra akaenda hadi robo fainali.

Henock Inonga wa Simba ndiye mchezaji pekee wa Ligi Kuu ya Tanzania aliyenusa hatua ya nusu fainali ya AFCON na kutolewa na wenyeji, Ivory Coast kwa bao 1-0.

Hapo utaona kuwa Ligi ya Tanzania kwa sasa ina heshima kubwa, ikichezwa na wachezaji wenye ubora na hadhi ya juu, hivyo inabidi hadhi hii ilindwe kwa nguvu zote.

Nimeanza kuona vitu vinavyoashiria kuanza kurudi kule kule tulikotoka.

Kuamini imani za kishirikina na kutoiheshimu nembo ya ligi si jambo lenye afya kwa ustawi wa ligi na mpira wetu.

Katika mechi mbili, Yanga ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji na Mashujaa FC kuna baadhi ya wachezaji wameonekana kwenda langoni na kupora taulo.

Katika mechi dhidi ya Dodoma Jiji aliyefanya hivyo ni Clement Mzize na mechi dhidi ya Mashujaa FC, kazi hiyo ilifanywa na Kibwana Shomari.

Kwa bahati mbaya sana waliofanya hivi wote ni wachezaji wa Kitanzania na si wa kigeni.

Hapa inaonyesha kuwa inawezekana wachezaji wetu wanaamini sana ushirikina zaidi tofauti na wachezaji wa kigeni ambao wanaonekana kujituma zaidi uwanjani.

Sitaki kwenda mbali kuhusu hilo, lakini napenda kuikumbusha Bodi ya Ligi iwe makini na hili jambo ambalo limeanza kujitokeza na wala tusipepese macho, ni kuchukua hatua.

Iwapo litanyamaziwa kimya, tutaanza kuona na wachezaji wengine na timu mbalimbali wanafanya hivyo na sasa itakuwa tena ni vurugu siyo mpira.

Bodi ya Ligi ina Mamlaka ya kuchukua hatua pale inapoona ligi yake ambayo ilitumia muda mrefu kuipa hadhi leo inachafuliwa kwani siku hizi inaangaliwa kwenye nchi nyingi sana Afrika, wanapoona wachezaji wanapora mataulo kwa kuamini imani za kishirikina ni kama kulipaka matope soka la letu.

Kinachoonekana, kinanikumbusha mechi za zamani uswahilini ambapo mtu anaweza kuingia uwanjani na kufanya chochote, na hata mchezaji pia anaweza kuamua lolote na asifanywe chochote.

Siku hizi hata kwenye Ndondo Cup, na mechi za uswahilini huwezi kukuta vitu kama vile kwa sababu hata mashabiki nao wameimalika sana kutokana na kufuatilia mechi za Ulaya.

Kazi kwenu Bodi ya Ligi, kusuka au kunyoa.

## RC atoa namba ya simu kupata taarifa ulanguzi bei ya sukari

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ametaja namba yake ya simu hadharani kwa lengo la kupewa taarifa kutoka kwa mwananchi yeyote atakayeuziwa sukari tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,700 hadi 3,200.

Amesema kwa mfanyabiashara yeyote atakayebainika anauza bei ya sukari tofauti na ile iliyopanga atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Malima alitoa namba yake jana wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) iliyofanyika kimkoa katika Manispaa ya Morogoro.

Katika maadhimisho hayo, mgeni rasmi alikuwa mlezi wa CCM Mkoa wa Morogoro ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa, Mohamed Ally Kawaida.

Malima alisema licha ya mkoa wa Morogoro kuwa na viwanda vinne vya sukari vikiwamo vya Mtibwa, Kilombero I na II pamoja na kiwanda kipya cha Mkulazi, kuna tatizo la upungufu wa sukari, hali iliyoilazimu serikali kuagiza tani 100,000 kutoka nje.

Alisema tayari awamu ya kwanza ya shehena ya sukari kutoka nje imeshawasili, huku serikali ikitoa bei elekezi ya kuuzwa kwa Sh. 2,700 mpaka 3,200 kulingana na maeneo na kwamba bei hiyo ni sheria, hivyo wafanyabiashara wote wanapaswa kuuza kwa kuzingatia bei hizo.

"Nawakumbusha wafanyabiashara serikali tayari imetoa maelekezo mahususi kuwa sukari inauzwa mwisho Sh. 3,200 kwa kilo na mwananchi akikuta anauziwa Sh. 3,500 anipigie simu mimi mwenyewe kwa namba yangu 0784 612020 nitaenda mara moja kushughulika nao," alisema Malima.

Alisema upungufu wa sukari uliojitokeza nchini umechangiwa na viwanda kushindwa kuvuna miwa kutokana na mashamba kujaa maji kulikosababishwa na mvua za mafuriko.

"Mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Morogoro. Nazunguka maeneo hayo kila siku na nimejionea viwanda vya Kilombero I na II, Mtibwa na Mkulazi mashamba yao yote yamezingirwa na maji na hakuna mashine wala trekta inayoingia shambani," alisema Malima.

Akizungumzia uhaba wa sukari, Kawaida alisema Baraza Kuu la UVCCM liliazimia kuhusu bei ya juu ya sukari inayoendelea kuuzwa nchini na wafanyabiashara na kuiagiza serikali ilishughulikie suala hilo.

"Mkuu wa Mkoa uliposimama hapa umetoa namba yako ya simu kwa wananchi. Umekiri wewe kwamba unafahamu hata mimi ninazo taarifa kwamba hapa Morogoro wapo baadhi ya wafanyabiashara wanauza sukari kwa bei ya juu tofauti na iliyopangwa na serikali," alisema.

Kaiwada alisema licha ya Malima kutoa namba yake ya simu kwa wananchi, alimwomba yeye pamoja na wakuu wa wilaya mkoani Morogoro, watoke ofisini kwenda kufanya msako kuwabaini wafanyabiashara wanaouza sukari kwa bei ya juu.

"Tokeni ofisini msisubiri kupigiwa simu. Nendeni mkafanye msako kukamata wafanyabiashara wanaouza sukari kwa bei isiyo elekezi ili kukomesha tatizo hilo,"

# Waziri akemea ukatili kwa watoto mtandaoni

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amekemea ukatili wa watoto mtandaoni na kuwataka wazazi na walezi kusimamia malezi mema ili kulinda kizazi kijacho.

Alisema hayo wakati akifungua mafunzo kwa wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana ambayo yalihusu ukatili dhidi ya watoto.

Dk. Gwajima alisema wazazi na walezi wanapaswa kuhimiza watoto wao matumizi sahihi ili wanufaike na fursa zilizopo mtandaoni.

"Tuweke wazi kuwa katika matumizi ya mitandao hiyo, wanaweza kukabiliana na aina tofauti za ukatili na unyanyasaji wa kingono," alisema.

Waziri Gwajima alitaja baadhi ya aina ya ukatili na unyanyasaji wa kingono mtandaoni ambazo mtoto anapaswa kuzifahamu kuwa ni picha, video na vitabu vya katuni.

"Katuni na vingine vingine vingi vinavyoonyesha sehemu za siri za mtoto au watoto wakinyanyaswa kingono, lakini pia kuna udhalilishaji na vitisho kwa kutumia picha," alisema.

Alisema kukua kwa teknolojia kumerahisisha mawasiliano, na kwamba watu wanaweza kuwasiliana ndani na nje ya nchi.

"Lakini wakati mwingine wanaweza kuwasiliana na watu wanaowajua au wasiowajua na kujikuta wakikumbana na ukatili wa mtandaoni.

Alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kusaidia kuelimisha kuzingatia malezi mema, kwa ajili ya kuepusha ukatili huo.

Mtaalamu wa Usalama Mtandaoni na Uchunguzi wa Kidijitali, Yusuph Kileo, alisema ni muhimu watoto kutumia mitandao, huku wazazi na walezi wakiwafuatilia kwa karibu.

"Mitandao ina programu nyingi zikiwamo zile ambazo hazifai kwa watoto, hivyo ni wajibu wa wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao hawaangalii programu zisizowafaa,"



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akizungumza katika uzinduzi wa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari kuhusu ukatili dhidi ya watoto mtandaoni jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mtaalamu wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto kutoka UNICEF Tanzania, Joseph Matikbwi na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya wizara hiyo, Mathias Haule. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ofisa wa TAKUKURU aeleza mshtakiwa alivyotoa rushwa mil. 10/- kwa ofisa polisi

**Na Grace Gurisha**

OFISA Uchunguzi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Agness Msumari, ameieleza mahakama kuhusu mwanamama Hawa Kirumbi (42) alivyotoa rushwa ya Sh. milioni 10 kwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa Jinai Mkoa wa Kinondoni, Mrakibu Msaidizi (ASP) Abdallah Nindi, ili kusitisha upelelezi wa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha usiendelee.

Aidha, amedai katika uchunguzi wake alibaini kuwa Kirumbi alikwenda Kituo cha Polisi Oysterbay katika ofisi ya ASP Nindi akiwa ameambatana na mwenzake aliyefahamika kwa jina la Rukia ambaye alimsubiri mshtakiwa nje huku akiwa amebeba fedha hizo.

Msumari alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemalila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi dhidi ya Kirumbi anayeshtakiwa kwa madai ya kutoa rushwa.

Alidai kuwa anakumbuka Oktoba 4, 2022 alikuwa ofisini kwake akiendelea na majukumu yake ya kazi, akapata maelekezo kutoka kwa mkuu wake kazi kwamba kuna taarifa imeletwa kwa njia ya barua kutoka ofisi ya ASP Nindi kuhusiana na Hawa Kirumbi kutoa rushwa ya Sh. milioni 10, hivyo anatakiwa aifanyie kazi.

"Fedha hizi alipewa ASP Nindi ili kusitisha upelelezi uliyokuwa ukiendelea katika ofisi yake dhidi ya tuhuma iliyokuwa inamkabili Laurian Severine Swai ambaye alikuwa ana kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha," alidai.

Msumari alidai kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, aliandaa mpango kazi kwa ajili ya kufanya uchunguzi na alianza kwenda katika Kituo cha Polisi Oysterbay, ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa Jinai kwa ajili ya kujiridhisha kama kuna tuhuma hizo.

Alidai kuwa Septemba 18, 2023 aliandaa barua kwenda kwa ASP Nindi kwa ajili ya kuomba vielelezo vya ushahidi pamoja na anwani ya watuhumiwa na siku hiyo hiyo, alipokea barua kutoka kwa ofisa huyo ikiambatana na watuhumiwa ambao walikabidhiwa ofisi kwao.

"Oktoba 24,2023 nilikwenda ofisini kwa ASP Nindi kwa ajili ya kufuatilia vielelezo, nilikabidhiwa barua pamoja na Sh. milioni 10, noti za Sh. 10,000 zilizokuwa 999 na noti mbili za Sh. 5,000. Nilizihakiki fedha hizi na kisha nilikabidhiwa na mtunza vielelezo aliyeitwa Afande Juma," alidai Msumari.

Ofisa huyo aliendelea kudai kuwa katika uchunguzi wake alibaini kwamba ni kweli kulikuwa na kiasi hicho cha fedha na ni kweli Kirumbi alikwenda kituo hicho cha polisi akiwa na Rukia ambaye alimwacha kwenye korido na baada ya muda kidogo, alitoka nje na kisha wakaingia wote kwenye ofisi ya ASP Nindi ambako alichukua fedha kutoka kwa Rukia na kumkabidhi.

"Katika uchunguzi wangu nilibaini fedha hizi zilikuwa rushwa na baada ya kumaliza uchunguzi, niliwahoji baadhi ya mashahidi nikishirikiana na mwenzangu aliyemhoji Rukia Abdallah," alidai.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 20, 2024 kwa ajili ya shahidi kuulizwa maswali ya dodoso na wakili wa mshtakiwa, Peter Kibatala.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa anadaiwa Julai 18, 2021 akiwa Kituo cha Polisi Oysterbay, Kinondoni, Dar es Salaam, alitoa rushwa ya Sh. milioni 10 kwa ASP Nindi ili kusitisha upelelezi wa kesi ya Swai ambaye alikuwa amekamatwa kwa tuhuma za unyang'anyi wa kutumia silaha.

# Mbaroni tuhuma wizi vifaa hospitali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linawashikilia watu wanne wakiwamo watumishi wawili na mlinzi mmoja kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya ujenzi katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP), Butusyo Mwambelo, alisema tukio hilo lilitokea Januari 31, mwaka huu, majira ya jioni katika Kata ya Mlowa.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni daktari ambaye alikabidhiwa funguo za stoo na mtunza stoo ambaye alikabidhiwa kutunza vifaa hivyo vya ujenzi.

Pia alisema mlinzi naye alikamatwa baada ya kupekuliwa nyumbani kwake na kukutwa na baadhi ya vifaa vya ujenzi vya hospitali hiyo.

"Kweli tukio la wizi limetokea likafunguliwa jalada la uchunguzi na mkurugenzi kuunda kamati ya ufuatiliaji wa jambo hilo ikaonekana vifaa vya ujenzi na umeme," alisema Mwambelo.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuchunguza tuhuma za wizi wa vifaa hivyo vya ujenzi ili kuwabaini wahusika wa tukio hilo.

Baadhi ya wananchi hao, Jackson Mlelwa na Ezekia Chongolo, walisema kuwa inaleta kichefuchefu kuona serikali inanunua vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo ili waweze kunufaika, lakini baadhi ya watu walioaminiwa wanafanya vitendo visivyofaa vya kuihujumu serikali.

"Mali nyingi zimeibiwa hapa Hospitali ya Mlowa na havikuibiwa nje bali kwenye stoo ambayo wanatunza madaktari wenyewe," alisema Chongolo.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Dk. Alexander Mchome, alisema ni kweli wizi huo umetokea lakini kuna utaratibu wa kutoa taarifa na anayeruhusu kulizungumzia suala hilo ni Mkurugenzi wa Halmashauri.

"Unatakiwa kuomba hicho kitu kwa kuandika barua akiridhia basi anayehusika kutoa hizo taarifa atakupa hizo taarifa, tukio lipo ila wasiliana na ofisi ya mkurugenzi akiruhusu tutakusaidia," alisema Mchome.

Diwani wa Mlowa, Odilo Fute alikiri kuwa vifaa hivyo vimeibiwa lakini jambo hilo lipo kwenye vyombo vya ulinzi na usalama kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

"Taarifa hizi nimezipata ilikuwa Ijumaa kwamba kuna tukio limetokea kuna vitu vimeibiwa hu kwa maelezo milango haijavunjwa ni kama kuna watu wamefungua na kutoa vitu ndani," alisema Fute.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mlowa, Hangaika Ngohonzela, aliiomba serikali kufanya uchunguzi wa haraka ili watakaobainika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Alisema: "Lazima uchunguzi ufanyike kwani kama hospitali haijavunjwa na vitu vinaonekana havipo na wenyewe wapo hapo hapo inawezekana ni wataalamu ambao wanajua kwamba pale kuna moja, mbili, tatu ndiyo maana hili jambo lipo kisiri zaidi."



Mkurugenzi Mtendaji wa Bank of Africa Group, Amine Bouabid (kulia), akiongozana na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Ghana, Kobby Andah (wa pili kulia) na Makaimu Wakurugenzi Watendaji wa benki hiyo Tanzania, Samir Yassine (wa pili kushoto) na Wasia Mushi (kushoto), wakiwa katika mazungumzo na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, Naibu Gavana, Sauda Kassim Msemo, Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha (BoT), Sadati Mussa katika makao makuu ya Benki Kuu ya Tanzania, jijini Dar es Salaam. Wengine ni Maofisa Waandamizi wa Benki Kuu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Taasisi 96 za umma zaunganishwa NIDA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa taasisi 96 za serikali na binafsi zimeunganishwa na Kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Welezo (CCM), Maulid Saleh Ali.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali imefikia hatua gani ya kuziunganisha taasisi zote za umma na binafsi na mfumo wa NIDA.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema kati ya taasisi hizo 44 ni za serikali na 52 ni za binafsi.

Sagini alisema moja ya majukumu ya NIDA ni kuanzisha na kutunza kanzidata ya taarifa za watu na kushirikishana taarifa hizo na taasisi zingine za umma na ili kutatua changamoto za utambuzi katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiusalama.

Alisema mpango wa NIDA ni kuendelea kutoa elimu na kuunganisha taasisi 200 ifikapo Juni mwaka 2026.

"Kasi ya uunganishaji inatarajiwa kuongezeka kufuatia utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Agosti 10, 2023 ya kutumika kwa namba moja (namba jamii) katika kumtambua mtu wakati wa kumpatia huduma badala ya mtu mmoja kuwa na namba zaidi ya moja," alisema.

# Naibu Waziri ataka hekima itumike masuala ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ametaka hekima itumike katika kushughulikia masuala ya ardhi kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka huku ardhi ikibaki ile ile.

Pinda alitoa kauli hiyo juzi wakati akijibu hoja za wabunge katika kikao cha Bunge kujadili Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kipindi cha Februari 2023 hadi Januari 2024.

"Lakini jambo moja ningependa niwaambie Watanzania wote, ardhi ya Tanzania kwa ujumla wake haina nyongeza yoyote. Tunayo tangu miaka ya 1950 mpaka sasa na haitaongezeka," alisema.

Kwa mujibu wa Pinda, miaka ya 1950 idadi ya Watanzania ilikuwa chini ya watu milioni tisa na sasa imefikia milioni 61, hivyo ni lazima hekima itumike katika kupitia mambo yanayoongoza sekta ya ardhi.

Alisema ongezeko la idadi ya watu ni moja ya sababu za kusukumana kwa Watanzania katika maeneo yao na aliwashukuru wabunge wanavyochangia mawazo ya jinsi ya kukabili ongezeko la watu bila ongezeko la ardhi.

Aidha, Pinda alisema wizara iko mbioni kujenga ofisi za ardhi za mikoa sambamba na kuwa na ofisi za makamishna wa ardhi wasaidizi wa wilaya.

Alisema kumekuwa na mtengano wa kimawasiliano kati ya maofisa wa wizara ya ardhi kwenye halmashauri walio chini ya wizara na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi mkoa.

"Tunaenda kuwa na makamishna wa ardhi wa wilaya ili kusimamia halmashauri zilizo chini ya wilaya jambo ambalo litasaidia kusogeza huduma za sekta ya ardhi karibu na wananchi.

"Kuhusu ongezeko la fedha kupitia mkopo wa Benki ya Dunia ambao moja ya kazi zake ni kufanya maboresho katika eneo la utawala wa wizara, niwahakikishie wabunge kuwa mikoa yote itapata majengo sambamba na kuanzisha ofisi za ardhi za wilaya ambazo kwa miaka yote haijawahi kutokea," alisema.



# Wenye ualbino wapatiwa msaada

Na Paul Mabeja, DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Stella Ikupa ametoa msaada kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) mkoani hapa, ikiwemo mafuta maalum ya kuwalinda na mionzi ya jua dhidi ya saratani ya ngozi.

Ikupa alikabidhi msaada huo jana jijini hapa kwa Mkurugenzi wa Shirika linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu la Foundation For Disabilities Hope (FDH) , Maiko Salali.

"Leo nimekuja hapa kukabidhi msaada huu kwa watu wenye ulemavu, vitu hivi ni mafuta maalum kwa watu wenye ualibino, kofia na miwani ambavyo vitawasaidia kujilinda na mionzi ya jua na kuondokana na tatizo la saratani ya ngozi," alisema Ikupa

Alisema vifaa hivyo ni muhimu kwa kulinda afya zao na kuwaomba wadau kujiwekea utaratibu wa kusaidia kundi hilo mara kwa mara.

"Hivi vitu kwa watu wenye ulemavu ni kama chakula kwao, mara nyingi watu wamekuwa wakihoji kwanini msaada kila siku, lakini sisi watu wenye ulemavu vifaa hivi ni kama chakula kwetu, hivyo ni wa muhimu kwetu," alisema Ikupa

Ikupa ambaye pia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Ikupa Trust Fund, alitoa wito kwa wadau kuendelea kusaidia makundi ya watu wenye uhitaji, wakiwemo walemavu.

Aliipongeza serikali kwa jitihada za kuwezesha makundi ya watu wenye ulemavu na kuwa mstari wa mbele kuweka mazingira rafiki kwa kundi hilo nchini ikiwemo kuboresha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kupitia mapato ya ndani ya halmashauri.

"Hivi karibuni bungeni kupitia swali langu serikali ilieleza kuwa ipo kwenye mchakato wa kuchambua takwimu za watu wenye ulemavu kupitia sensa ya watu na makazi iliyofanyika 2022 ili kupata idadi kamili itakayowezesha kuhudumia kundi hilo kikamilifu," alisema

Mkurugenzi wa FDH, Maiko Salali, alimshukuru mbunge huyo kwa msaada huo akisema utawasaidia watu wenye ualbino mkoani hapa.

# DC asambaratisha kikundi cha ulinzi

Na Thobias Mwanakatwe, MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali ameagiza kuvunjwa kikundi cha ulinzi cha Nkiri kilichoanzishwa Kijiji cha Yulansoni wilayani hapa Mkoa wa Singida kwa kukiuka sheria kwa kutoa hukumu na kutoza faini wananchi. Kikundi hicho ambacho kimeleta taharuki kwa wananchi na kuhatarisha usalama wa maisha yao, kimekuwa kikiwatenga kununua bidhaa kwenye maduka yaliyopo kijiji hicho, kuchota maji na kutoruhusiwa kusaga nafaka katika mashine.

Adhabu hizo zimekuwa zikitolewa kwa mwananchi anayebainika kutenda kosa na kikundi hicho kwa kushirikiana na Serikali ya kijiji.

Machali akitoa taarifa kwa waandishi jana wakati wa kikao cha Baraza la Ushauri la Wilaya hiyo, alisema taarifa za kuwepo kwa kikundi hicho alizipata baada ya mwananchi mmoja kulalamika kutengwa na kikundi hicho ambacho kinashirikiana na Serikali ya kijiji hicho.

"Mwananchi Henry Singano alinipigia simu na kuniandikia barua ametengwa na kikundi cha ulinzi cha Nkiri na serikali ya kijiji haruhusiwi kununua bidhaa dukani, kusaga nafaka mashineni wala kuchota maji mabomba ya kijiji," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya, alisema pia kikundi hicho kilimtoza mwananchi huyo faini shilingi 3,264,000 kwa madai ya kukiuka kukodi shamba kwa mwalimu mali ya kijiji.

Machali, alisema kufuatia malalamiko ya mwananchi huyo na wengine, alikwenda katika kijiji hicho akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na kuitisha mkutano ambapo wananchi walikilalamikia kikundi hicho kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

"Ni kosa kumtenga mwananchi yeyote na kama amefanya kosa afikishwe kwenye vyombo vya sheria, hivyo kuanzia sasa ni marufuku kikundi cha ulinzi cha Nkiri kufanya shughuli zake kwenye kijiji hiki," alisema.

Katika mkutano huo, watu watatu wanaoaminika washiriki wa kikundi walikamatwa na Jeshi la Polisi.



Stella Ikupa (kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa niaba ya watu wenye ulemavu wa mkoa wa Dodoma kwa Mkurugenzi wa shirika linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu la Foundation For Disabilities Hope (FDH), Maiko Salali, jijini Dodoma jana. **PICHA PAUL MABEJA**

# TAKUKURU wachunguza miradi mabilioni

Na Paul Mabeja, DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imechunguza utekelezaji miradi 35 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 21.16 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa huo, Asha Kwariko akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, aliitaja baadhi ya miradi hiyo na idadi yake kwenye mabano kuwa ni ya elimu (24), ujenzi (minne), afya (mitatu) na maji (minne).

"Katika ufuatiliaji huu miradi ya elimu ilikuwa ni miradi yetu ya kipaumbele kwa sababu mwezi Januari tulitarajia wanafunzi wapya wa kidato cha kwanza wengi zaidi wasajaliwe kama ilivyo kwa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa shule za msingi," alisema Kwariko

Alisema katika ufuatiliaji huo, walibaini mapungufu katika miradi 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 4.34.

Alisema pamoja na utekelezaji wa majukumu ya kawaida, wamejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele vinavyolenga kuzuia vitendo vya rushwa visitokee.

"Malengo hayo ni pamoja na kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuziba mianya ya rushwa na ufujaji fedha unaoweza kujitokeza katika utekelezaji miradi hiyo.

"Hii ni pamoja na kufuatilia miradi ya ujenzi wa madarasa, vituo vya afya na miradi mingine ambayo bado inaendelea kujengwa kupitia fedha za kuimarisha elimu ya awali na msingi na kufuatilia kero za migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikilalamikiwa kila kukicha," alisema

Kadhalika, alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo lakini bado wapo baadhi ya watu wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya ubadhirifu.

"Ndiyo maana katika malengo yetu tumeweka nguvu kwenye ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayotumia fedha nyingi za serikali ili kuzuia vitendo vyote vya rushwa," alisisitiza

Aliyataja malengo mengine kuwa ni kuongeza kasi ya uelimishaji umma kwa kutumia njia mbalimbali hasa katika makundi ya vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa.

"Pamoja na kuzindua shindano la mdahalo wa uelimishaji rushwa juu ya madhara ya rushwa katika shule za sekondari na vyuo vikuu vilivyopo Wilaya ya Dodoma, tutaendelea kuelimisha jamii hususani vijana kupitia ushirikiano uliopo kati ya TAKUKURU na Tume ya kudhibiti dawa za kulevya na jamii nzima ya Wanadodoma," alisema

Alisema, kipaumbele kingine ni kuongeza kasi ya kufanya uchambuzi wa mifumo hasa maeneo yanayolalamikiwa zaidi katika utoaji wa huduma kwa wananchi na miradi inayogusa jamii.

"Vilevile tumepanga kufanya uchunguzi katika tuhuma zilizoainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), malalamiko ya matumizi mabaya ya ofisi na mamlaka katika Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma na zingine kadri zitakavyobainika," alisema



# JKCI kutoa matibabu ya moyo A. Kusini

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amemwagiza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuandaa mpango wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kutolea matibabu ya moyo Afrika cha Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) .

Dk. Mpango alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mkutano wa madaktari wa moyo unaofanyika visiwani hapa.

Alisema kuwa anamwagiza waziri huyo kusaka wadau hao na fedha za kufanikisha ujenzi wa kituo hicho kama alivyoomba Mkurugenzi wa JKCI, Dk. Peter Kisenge.

Awali, Dk. Mpango, alisema serikali itaendelea kuwekeza katika sekta ya afya ili kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Alisema serikali inatenga wastani wa Shilingi bilioni 63 katika taasisi hiyo na kuiwezesha kutoa huduma za matibabu, kupunguza vifo na athari nyingine zinazosababishwa na magonjwa ya moyo.

"Kutopewa kipaumbele kwa maradhi yasiyo ya kuambukizwa katika nchi nyingi za Afrika kumechangia ongezeko la maradhi ya moyo. Natoa rai kwa JKCI na watoa huduma za afya kuendelea kutoa elimu ya namna ya kujiepusha na mambo yanayochangia magonjwa ya moyo," alisema Dk. Mpango.

Alipongeza juhudi zinazochukuliwa na JKCI kutoa elimu kwa madaktari na kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi

Aliwataka washiriki wa mkutano huo kutumia fursa ya mafunzo na maelekezo yatakayotolewa na wataalamu na madaktari wabobezi na kwenda kutumia katika nchi zao.

Awali Dk. Kisenge alisema kuwa taasisi hiyo ina lengo la kupanua huduma zake kwa kuanzisha kituo cha matibabu ya moyo kwa nchi za Afrika.

Alisema ndoto hiyo itakapokamilika, itachochea utalii wa matibabu na kupunguza gharama za matibabu ya moyo kwa wananchi wa mataifa ya Afrika hasa ya nchi jirani na Tanzania.

Alisema JKCI imeanzisha mpango wa umahiri katika hospitali za kanda za KCMC, Bugando, Mbeya, Benjamin mkapa (Dodoma) na Chato ili kufikisha huduma zaidi kwa wananchi.

"Kupitia mpango huu katika mwaka uliopita na mwanzoni mwa mwaka huu, tumefanikiwa kufanya kambi maalumu za matibabu katika mikoa zaidi ya 10 na pia nchi za Zambia, Rwanda na Malawi," alisema Kisenge.

Alisema mafanikio hayo yametokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwa taasisi hiyo, hivyo kupunguza rufani za matibabu ya moyo nje ya nchi kwa asilimia 95.

Waziri Ummy, alisema serikali imeendelea kuwekeza katika kuipatia taasisi hiyo vifaa vya kisasa vya matibabu na vya kutolea huduma.

Alisema pamoja na ongezeko la magonjwa hayo yasiyo ya kuambukiza nchini na mataifa mengine ya Afrika, ipo haja ya watoa huduma za afya kuwekeza zaidi katika elimu ya afya na kinga ili kuyadhibiti.

"Maradhi yasiyoambukiza yakiwamo ya moyo yanazuilika. Hapa nataka kutilia mkazo juu ya watu kutofanyia mzaha mafunzo yanayotolewa na Profesa Mohamed Janabi (Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili) kuhusu ulaji sahihi na matumizi ya vitu vyenye kuathiri afya ikiwamo uvutaji sigara na unywaji pombe kupitiliza," alisema.

Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan khamis Hafidh, alipongeza juhudi zinazofanywa na JKCI na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutanua wigo wa upatikanaji wa matibabu ya moyo nchini.

Hafidh, alisema Serikali ya Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitatu, imejenga hospitali 10 za wilaya, moja ya mkoa na kuzipatia vifaa vya kisasa ili kuimarisha huduma za afya nchini.

Mkutano huo wa siku mbili ulioanza kwa mafunzo kwa wataalamu na madaktari wa magonjwa ya moyo kutoka nchi 40 za ndani na nje Afrika, unatarajiwa kufungwa leo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kauli mbiu ya mkutano huo ni 'Maendeleo katika utoaji huduma za matibabu ya moyo Afrika'.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akimwagilia mti aina ya mpilipili doria, baada ya kuupanda wakati wa zoezi la upandaji miti kuhamasisha utunzaji mazingira katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume Zanzibar jana. **PICHA: OMR**

## Serikali, kampuni za kilimo kushirikiana

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itaendelea kushirikiana na kampuni ili kuinua kilimo nchini.

Hayo aliyasema jana katika Kijiji cha Chwaka Wilaya ya Kati Unguja wakati akitembelea shamba la Kampuni ya AATIF Aquaponics inayojishughulisha na kilimo zinafanywa bila kutumia udongo.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kutambua jitihada zinazofanywa na kampuni hiyo na kuona teknolojia wanazotumia katika uzalishaji wa kilimo hicho.

Alisema wizara yake imefarijika kuona teknolojia hiyo inavyofanya kazi kwa lengo la kuhakikisha wana mkakati wa uzalishaji wa kilimo biashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Rashid Ali Rashid, alisema wanakabiliwa na changamoto kwa upande wa wadau katika taasisi za serikali na binafsi kutokana na kutofahamika kilimo hicho.

Rashid, aliiomba serikali na wadau kuwapa ushirikiano katika kilimo chao na kuishauri kutengeneza sera ya kilimo ili kuiwezesha jamii kufahamu umuhimu wa kilimo cha kisasa kinachotekelezwa katika shamba hilo lenye ukubwa wa kilomita 1,000 lenye mazao yapatayo 6,000.

# Watendaji waagizwa kuwaelimisha sheria za wavuvi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Shaabani Ali Othman, amewataka watendaji wa wizara hiyo kuwaelimisha wavuvi sheria za uvuvi na kukabiliana na uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi.

Alisema hayo jana ukumbi wa Mkutano wa Soko la Samaki Malindi Wilaya ya Mjini Unguja wakati akizungumza na wavuvi na kamati za Uvuvi za Wilaya ya Magharib 'A' na 'B'.

Alisema wavuvi watakapopewa elimu ya sheria wataondokana na migogoro kati yao na wakuu wa taasisi katika utumiaji wa bahari.

Aliwaagiza wakuu wa taasisi kuacha kuwachangisha fedha kiholela wavuvi na kuondoa sintofahamu kati yao na watendaji.

Vilevile, aliwaagiza watendaji kuwapatia leseni wavuvi, lasivyo wawarejeshee fedha zao.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema kwa mujibu wa sheria ya uvuvi ya mwaka 2010, mtumiaji wa fukwe atalazimika kuacha mita kumi kwa eneo la majabali ili wavuvi wapate maeneo ya kufanyia shughuli zao.


Alisema wizara hiyo imegawa boti 530 na hivi karibuni inatarajia kugawa nyingine zaidi ya 800 kwa wavuvi na wakulima wa mwani. Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sudi Hamed, alisema wizara yao inatarajia kuanzisha mfumo wa kidijitali kwa wavuvi ili kudhibiti uvuvi haramu visiwani hapa.

Alisema Wizara hiyo pia inatarajia kutoa leseni kwa njia za elektroniki ili kuondoa urasimu wa baadhi ya watendaji waliopewa mamlaka hayo.

Mkurugenzi Idara ya Uhifadhi na Bahari, Dk. Makame Omar Makame, aliwataka wavuvi kutoa taarifa dhidi ya uvuvi haramu hasusani katika maeneo ya hifadhi ya bahari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uvuvi eneo la Kihinani, Omar Mwinyi Mpango aliiomba wizara hiyo kuwapatiwa boti za doria kwa ajili ya kuwafuatilia wanaojihusisha na uvuvi wa kutumia mabomu kwa kuwa unaathari mazingira.

Mwalimu Suleiman Hamada kutoka Buyu, aliitaka wizara hiyo kufuatilia wavuvi wanaotumia nyavu za kukokota ili kunusuru mafungu baharini.



TAYLOR UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI ...ELE
JUMAMOSI FEBRUARI 10, 2024



# DAH! HIYOO IMETOBOA

WIMBO mpya uliowashirikisha wanamuziki nyota wa Bongo Fleva, Nandy na Ali Kiba, unazidi kuwaziba midomo wapinzani wao upande wa pili, baada ya kufanya vizuri nje ya mipaka ya Tanzania.

Wimbo huo unaoitwa 'Dah' ambao ameutambulisha mwanzoni mwa mwezi huu, umekuwa kama umeanza kumwonyesha njia kupasua anga za kimataifa kutokana na mashabiki wa muziki wa ndani na nje ya Tanzania kuupokea vizuri.

Katika kile kinachoonekana msanii huyo amecheza karata yake vyema, ni baada ya wimbo huo unaozungumzia mahaba kushika namba moja katika majukwaa ya muziki ukiwepo mtandao wa YouTube.

Katika jambo la kufurahisha zaidi msanii wa Marekani, Usher Raymond , ameonekana kuvutiwa na kibao hicho kiasi ambacho ameomba kufanya kolabo ya remix ya wimbo huo.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Nandy amewataarifu mashabiki wake kwamba watarajie mambo mazuri kwani kuna ujio mpya wa wimbo huo na mwanamuziki huyo mkubwa.

Kimsingi Usher ndiye aliomba kufanya kazi na mwanadada huyo baada ya kumwandikia ujumbe akimtaarifu kuhusu uzuri na mvuto wa aina yake katika wimbo wake mpya 'Dah!' kiasi ambacho kinamnyima usingizi kama hawatafanya marudio.

Akielezea kutoka ndani ya moyo wake, Usher Raymond alimwambia kwamba wimbo huo umemkosha na kama anaweza basi amkubalia wakutane kwa ajili ya kufanya remix.

Nandy ameeleza kwamba hakusita kukubaliana na dili hilo na kwamba yuko tayari wakati wowote kufanikisha mpango huo ambao ameutaja zawadi njema kutoka kwa Mungu 2024.

BASI SAWA

## Ben Pol ashindwa kumlaumu Diamond

MWANAMUZIKI maarufu wa miondoko ya R &B, Ben Pol, amesema alishindwa kumshirikisha Diamond Platnumz katika wimbo wake



'Moyo Mashine' kutokana na uongozi unaomsimamia kutaka sehemu ya mapato.

Akizungumza na kituo cha radio cha East Africa juzi, Ben Pol amesema licha ya wimbo huo kushiba kila eneo, uongozi wa Diamond walitaka kupewa asilimia zinazotokana na haki ya kushirikishwa katika wimbo huo ambao ulikuwa maarufu.

"Diamond hakutaka nimpe pesa, lakini uongozi wake ulitaka tuwapatie sehemu ya haki ya wimbo baada ya kutoka, tulipofikiria sana tukaamua niimbe mwenyewe kwa sababu ulikuwa na kila kitu ambacho watu wangeupenda na ndivyo ilivyokuwa," Ben Pol.

## Itakuwa vipi Kajala kuitwa bibi?

Hebu fikiria, mwanamke mrembo kama Kajala vile, halafu akaitwa bibi. Kama mambo yataenda kama yalivyopangwa inawezekana ikawa hivyo.

Hii ni baada ya kuonekana kuwa huenda binti yake Paula akajifungua hivi karibuni.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja sasa, Paula na msanii Marioo wamekuwa katika kile kinachotajwa kuwa mapenzi mazito, huku Kajala mwenyewe akiliafiki penzi hilo.

Muigizaji huyo mkongwe wa filamu za Kitanzania amethibitisha kupitia ukurasa wake wa Instagram kwamba hivi karibuni ataitwa bibi.

"Ila Paula, muda wa kuwa bibi ulikuwa bado kidogo jamani," Kajala aliandika akiwa katika picha nzuri kwenye ufukwe wa bahari.

Maneno hayo yalimfanya mwimbaji mkongwe, Ray C naye kuandika kwenye akauti ya Kajala.

"Katutenda huyu mtoto, 'ngachoka.'"

Mwaka jana, Paula na mamake Kajala walithibitisha kwamba Marioo alikuwa amewasilisha mahari kwa ajili ya kumuoa kabisa mrembo huyo ambaye pia ni mjasiriamali wa mavazi.




# CHINO ANYANYUA MIKONO JUU

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Chino amesema hana kinyongo na Marioo na kwamba amefunga ukurasa hawezi kuzungumzia ugomvi wao tena.

Amesema licha ya kukwazwa na kilichokuwa kikiendelea kati yao, lakini ameamua kuyamaliza kwa sababu anatakiwa kuangalia mbele kuhakikisha anajikwamua kiuchumi.

"Mimi ni mtoto wa kiume ninapozungumzia jambo huwa baadae linaisha na kuendelea na maisha mengine.Tuangalie nini tufanye kufanya familia zetu ziishi badala ya kuendelea kulumbana," amesema Chino.



# Esma, usimwache ng'o

Msanii Esma amezama kwenye penzi jipya na mwanaume mmoja anayefahamika kwa jina la Jembe One, huku akisema hamuachi ng'o hata watu waseme nini.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Esma, ambaye ni dada wa Diamond Platnumz ameachia orodha ndefu ya sababu ya kwa nini hawezi kushawishika kumuacha mpenzi wake mpya ambaye wanatarajia kufunga harusi hivi karibuni.

"Simuachi mume wangu eti kisa kuna mtu kasema kachepuka naye, simuachi eti kisa kazaa nje, mtajuana wenyewe mnavyolea mtoto wenu kwa kujiibaiba," Esma alisema halafu akaongeza.

"Simuachi kwa kufikiria ndugu watanionaje au marafiki. Ninachojali mimi ni furaha yangu. Pia simuachi eti kisa hana hela, tutatafuta wote tutaleta mezani," akaongeza.

Esma alisema kwa umri aliokuwa nao yeye ndiye ana maamuzi anayoona yanafaa na si hayuko tayari kusikiliza chochote kutoka kwa familia, ndugu, jamaa wala marafiki kumhusu Jembe One.

Akamaliza kwa kuwashauri wanawake wenzake kwamba huku nje ni kugumu, watulie na wanaume walionao, wasihadaike kwani maisha ni magumu.

## DAH! NANDY MIDUME MITANO

**Na Adam Fungamwango**

MSANII maarufu wa kike nchini, Nandy, ameweka rekodi ya kuwa wa kwanza kwa wasanii wa kike kushusha ngoma 2024.

Februari 2, Nandy ametoa ngoma iliyoita 'Dah!' Ni wimbo ambao umeshaanza kuteka hisia za mashabiki kwani ndiyo unaoongoza kutazamwa kwa wingi na kushika namba moja kwenye mtandao wa 'Youtube.'

Hakuna rekodi yoyote inayoonyesha kuwepo kwa msanii wa kike wa bongo fleva kutoa ngoma yake tangu ulipoingia mwaka huu.


Katika pini yake hiyo, amemshirikisha mkongwe kwenye shughuli za muziki wa bongo fleva Ali Kiba na kumfanya kuwa mmoja wa wasanii wa kike nchini kuwashirikisha wasanii wengi wa kiume wa ndani na nje ya nchi kwenye ngoma zake.

Hizi ni ngoma tano ambazo Nandy amewahi kuzitoa, akiwashirikisha wasanii watano wa kiume.

**Nandy feat Alikiba - Dah!**

Huu ndiyo wimbo mpya wa Nandy ambao sasa unatamba kwenye vituo vya redio, televisheni na mitandao mbalimbali ya kijamii.

Ni wimbo wa kwanza kwa Nandy mwaka 2024, ambao amemshirikisha msanii Kiba na kuifanya kuwa na vionjo na ladha ya kuvutia masikioni.



**Nandy feat Harmonize - Acha Lizame**

Hii si mara ya kwanza na haitakuwa ya mwisho kwa msanii huyo kufanya kolabo na wasanii wa kiume kwani Juni 12, 2020, alifyatua ngoma moja kali iitwayo 'Acha Lizame' ambayo alimshirikisha mmoja wa wasanii wa kiume vipenzi na mashabiki wengi wa bongo fleva nchini, Harmonize.

**Nandy Feat Billnas - Do Me**

Mwaka huo huo, mwezi Oktoba, tarehe 17, 2020 alitoka studio akiwa amechia ngoma aliyoita 'Do Me' ambayo hii alimshirikisha msanii maarufu, Billnas.

**Nandy Feat Joeboy-Number One**

Kama ulidhani huwashirikisha wasanii wa kiume wa Kibongo tu basi unakosea. 2021, aliingia studio na Januari 7 akatoka na dude moja liitwalo, 'Number One', ambalo alimshirikisha msanii Joeboy kutoka Nigeria.

**Nandy Feat Koffi Olomide - Leo Leo**

Papa Mopao, mutu wa Congo, Koffi Olomide naye hakusalimika kwa Nandy, kaitwa nchini na kutengeneza ngoma moja kali iliyoitwa 'Leo Leo', ikafyatuliwa, Februari 16, ambayo ilitamba sana.

FILAMU

# Tatizo lako uzuri wako

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU inaitwa 'Tatizo Lako' inamhusu msichana mmoja aitwaye Penina aliyekuwa akikataa wanaume wengi wanaojitokeza nyumbani kwao kuleta posa.

Uzuri aliojaaliwa na Mwenyezi Mungu ulioonekana kumdanganya kuwa atabaki nao milele.

Mama yake naye akachangia kwa sababu alimfanya kitenga uchumi.

Kazi yao ilikuwa moja tu. Kuchukua barua za uchumba za wanaume kufungua na kutumia pesa walizoambatanisha ya kifunga uchumba. Wakaishi kwa staili hiyo. Baba yake Penina alikuwa ameshafariki miaka mingi iliyopita.

Muuza genge, Ibra, alionekana kumpenda sana Penina, lakini akashindwa na tabia zake, ikiwemo uvaaji wa nguo zisizo na stara.

Mara kwa mara Penina anapoenda gengeni kununua mahitaji, anakutaka na ushauri nasaha na maneno ya hekima kutoka kwa Ibra, huku akisifika kwa uzuri wake, lakini akamtaka kujisitiri. Penina hakupenda hilo.

Zilikuja barua kutoka kwa watu mbalimbali zilizowekwa Sh 30,000, zingine 50,000 na hata laki moja, lakini wote walikataliwa.

Aliyekuwa fukara alipondwa na hata aliyekuwa na pesa akaambiwa ana kiherehere.

Ukimya wa kutojibiwa barua zao ulisababisha wanaume karibia watano waliotoa barua zao za uchumba kutinga nyumbani kwa kina Penina kuulizia, lakini majibu yalikuwa ya nyodo.

Ndipo shangazi yake anawasili kutoka kijijini, na alipokaa siku mbili tu akaona kuna matatizo.

Wachumba wanakuja yeye, Penina hataki kuolewa na sababu kubwa ni mama yake.

Anampa somo Penina kuwa hata yeye alikuwa mrembo kuliko Penina, na ilimfanya kukataa wanaume wengi waliokuja kutaka kumuoa. Akawa hajui kuwa uzuri wa mwanamke ni kama ua, huchanua asubuhi na kunyauka jioni. Aliposhtuka akachelewa, uzuri ukaondoka, wanaume hawamtaki tena. Wanamkwepa. Mpaka sasa hajaolewa na wala hana mtoto.

"Uzuri wako ndiyo tatizo lako. Huo uzuri unaoringia sasa ndiyo baadaye utakufanya ujute na kukuletea matatizo." Akamwambia mtoto wa kaka yake.

Penina akamuelewa. Posa zikamiminika tena kama mvua. Penina akaacha wote, mpaka wenye uwezo wao. Akamchagua muuza genge. Yule aliyekuwa anamuasa kujisitiri. Na yeye safari hii alileta posa.



BURUDANI TELE




# Taylor Swift auza ndege yake

MSHINDI wa tuzo za Grammy 2024, Taylor Swift, ameuza moja ya ndege zake binafsi na kuanzisha kampuni yake mpya.

Taylor ambaye ni mwanamuziki nyota, aliuza ndege hiyo aina ya Dassault Falcon 900 mwezi uliopita baada ya kuwa nayo tangu 2009, akiitumia katika shughuli zake mbalimbali.

Fedha zilizotokana na mauzo ya ndege alizitumia kuanzisha kampuni hiyo mpya ambayo inahusika na biashara ya magari.



## Ufafanuzi anguko la Wanigeria

KAMATI ya utoaji wa tuzo za Grammy nchini Marekani, imetoa utetezi kuhusu malalamiko ya mashabiki wa muziki nchini Nigeria wanaodai wasanii wa nchi hiyo wamenyimwa ushindi kutokana na hila.

Tuzo 66 za Grammy zilitolewa Februari 5, 2024, katika jiji la Los Angeles, huku wasanii wa Nigeria Burna Boy, Davido, Asake & Olamide na Ayra Starr hawakupata hata moja.

Kulingana na Rais wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo cha Kurekodi Harvey Mason, amesema Chuo hicho hufanya tathimini kila wimbo kuhusu ubora wake na kupitia maoni ya washiriki wa chuo hicho ambao huamua washindi kila mwaka.

## Mwigizaji Ethel aaga dunia

MWIGIZAJI mkongwe na muhusika wa filamu ya Basi and Company, Ethel Adere-mi-Ekpe, ameaga dunia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Kitaifa ya Kudhibiti Filamu na Video (NFVCB), Dk Shaibu Husseini, ametangaza kifo cha msanii huyo maarufu nchini Nigeria ambaye alifariki juzi baada ya kusumbuliwa na saratani.

"Atakumbukwa sana na familia yangu kwani itamkosa kwa sababu tulimwita binti yangu wa pili Ethel," ameandika .





## Kanayo anachosema kizingatiwe

MWIGIZAJI wa Nollywood, Kanayo O. Kanayo amewashauri wazazi wa Nigeria kuhoji chanzo cha utajiri wa watoto wao.

Muigizaji huyo aliwasilisha ujumbe huo katika hafla moja aliyohudhuria na video fupi ya tukio hilo aliiweka kwenye ukurasa wake wa Instagram.


Katika tukio hilo Kanayo aliwaambia wazazi waliokuwa wakimsikiliza kwamba kuna umuhimu wa uchunguzi wa kina wa shughuli zanazowapatia fedha za watoto wao ili kuepuka hatari zinazoweza kutokea.

## Kanye West kuwaimbisha Wakenya

RAPA maarufu kutoka Marekani, Kanye West anatarajia kufanya ziara kimuziki kuzunguka mataifa mbalimbali duniani ikiwamo nchi za Kiafrika Nigeria na Kenya.

Kulingana na ratiba iliyotolewa na timu ya msanii huyo, Kanye West ataanza kwa kufanya tamasha kubwa nchini Canada na kufuatia msururu wa maonyesho katika majimbo yote ya Marekani mwezi Agosti.

Ziara hiyo itamfikisha nchini Mexico, Hispania, Misri, Uingereza, Falme za Kiarabu, Nigeria, Australia, Japan na kumalizia nchini Kenya Desemba 7, mwaka huu.





# Msuya: Viongozi epukeni migogoro

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Cleopa David Msuya, amewaonya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro kujiepusha na migogoro ili kulinda maslahi ya wakazi wa Mwanga.

Msuya alitoa kauli hiyo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa ofisi ya CCM Kata ya Kigonigoni wilayani hapa.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakiacha kazi zao na kujiingiza katika migogoro ya watu kwa maslahi yao binafsi na kuwataka viongozi kutotumika.

"Mmesikia hapa huyu kijana Rajabu Manyinya alipoanza kujitolea kwa ujenzi wa hii ofisi ya chama kata wapo watu wanafikiri anatafuta nafasi ya kugombea, wanaacha kazi zao na kuanza kumshughulikia," alisema na kuongeza kuwa:

"Chama kimesema kila baada ya miaka mitano mwanachama wa CCM ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, kitakachokuweka wewe milele katika nafasi yako ni jinsi utakavyotoa huduma nzuri kwa wapigakura wako."

Alisema watu wanaopita kueneza maneno ya uongo sio wa kufanya kazi wala kujitolea kwa ajili ya wapigakura wao na kwamba kama wangekuwa wamejitolea vizuri wasingekuwa na wasiwasi.

Msuya, alitoa wito kwa viongozi wa CCM kuwa imara kwa kudhibiti watu wanaoeneza uongo kwa wakazi wa Mwanga kwani kama wanatafuta nafasi ya kuchaguliwa ndani ya chama kuwa madiwani, mbunge na wadhifa mwingine, wanapaswa kufuata utaratibu.

"Ninyi chama ndio mnaopitisha majina ya wagombea, watu wenye tabia ya kueneza uongo futeni majina yao katika wilaya yetu ya Mwanga kwani mkifanya hivyo hakutakuwa na tatizo," alisema.

Alisema kinachofanyika ni sawa na kupoteza muda mwingi na fedha nyingi kuhonga kwa baadhi ya wanachama wa CCM ili waendelee kuchanguliwa bila ya faida yoyote.

Alisisitiza kuwa njia pekee ni chama kusimamia misingi yake na kama kuna watu wanapitapita na kutoa zawadi, kujitangaza na kipindi cha uchaguzi kinapofika wakati wa kupendekeza majina hayo yanafyekwa kwa kuanza kampeni mapema. Msuya alisema wanachama wa CCM Mwanga wataendelea na moyo wa kushirikiana, mshikamano, umoja a na kufuata mila nzuri za kipare.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Ibrahim Urio, alisema mwaka huu ni wa Uchaguzi wa Serikali za mitaa na kuwaasa wananchi na wanachama CCM kuchagua viongozi bora kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Urio alisema CCM ni chama pekee kinachoweza kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo na kuwaomba wawachague wagombea wake.

Mwenyekiti wa ujenzi wa ofisi hiyo, Rajabu Manyinya, alisema alipata wazo hilo ili kurudisha shukrani kwa CCM kwa yale yote aliyofanyiwa kupitia Msuya.

Alisema kada huyo alimsomesha sekondari hadi kuhitimu elimu yake ya juu.

Manyinya, alisema ujenzi wa ofisi hiyo unatarajiwa kugharimu Shilingi milioni 24 mpaka kukamilika kwake.

Msuya aliongoza harambee na kukusanya Shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo.



Maofisa wa Shirika la Misaada la Uturuki (Red Crescent Turkey) pamoja na Jukwaa la Wanawake wa Malkia wa Arusha, wakionyesha baadhi ya vitu kabla ya kukabidhi misaada mbalimbali kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania, kwa ajili ya waathirika wa mafuriko katika Kijiji cha Gendabi, wilayani Hanang', mkoani Manyara juzi, ambapo Balozi wa Uturuki, Dk. Mehmet Gulluoglu (hayumo pichani), alishuhudia makabidhiano hayo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Taasisi zaagizwa kuendeleza 4R

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI za Serikali zimeagizwa kuendeleza falsafa ya Rais Samia Hassan Suluhu ya 4R kutoa huduma kwa wananchi haraka kupitia Serikali Mtandao (e-GA).

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete wakati akifunga kikao kazi cha nne cha e-GA.

Rudhiwani aliwasisitiza maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufanya matumizi sahihi ya mtandao ili kuharakisha maendeleo kwa serikali na taasisi zake.

Alisema ni lazima e-GA izingatie sheria, viwango na sera kwa ajili ya ubadilishanaji taarifa za serikali salama. "4R ya Rais wetu ya kuhimiza ustahamilivu siyo kwa wanasiasa pekee bali kila nyanja kwa sababu mageuzi na ujenzi mpya wa maridhiano ni nguzo muhimu katika uletaji chachu ya maendeleo nchini, kuondoa changamoto za wananchi kupitia mifumo inayosomana na naziagiza taasisi za umma kusomana kupitia mifumo ya kidigitali," alisema.

Alisema kuna watu wanatumia barua pepe zisizo rasmi kutapeli wananchi katika ajira na malipo, hivyo wataalamu wa TEHAMA hasa serikali mtandao wanatakiwa kuwa kwa makini ili kuhakikikisha usalama wa mitandao unadhibitiwa.

" Kama kuna changamoto ya mifumo kutosomana ni wajibu zizungumzwe kuondoa ukakasi huo na kwenda pamoja katika ujenzi wa kidigitali, ikiwamo maofisa masuhuli kuwajengea uwezo wataalamu wa serikali kufikia malengo ya kidigitali," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha e-GA inafikia malengo na kutoa ufanisi wa kidigitali kupitia mfumo huo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya e-GA, Benedict Ndomba, alisema miradi ikiwa na mifumo ya TEHAMA, itasaidia kuokoa fedha za umma na za serikali.

"Tunamshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kujenga serikali kidigitali, lakini naomba Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa e-GA katika kuleta ufanisi zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa e-GA Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Said Seif Said, alipongeza ushirikiano baina Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajili ya kuhakikisha utendaji kazi ofisini unakuwa kwa kasi kupitia teknolojia hizo. Akisoma maazimio yaliyofikiwa kwenye kikao kazi hicho, Priscas Kiwango kuwa ni pamoja na kila taasisi kuteua ofisa TEHAMA kusimamia miongozo na kanuni za usimamizi bora wa mtandao, taasisi za umma ziboreshe na kutumia teknolojia hiyo.

Nyingine ni utoaji huduma kwa wananchi, kufanya tathmini ya hali ya TEHAMA, uundaji wa ripoti katika kila taasisi husika na kuwasilisha e-GA kabla ya mwaka wa fedha.

# DAS kusaka kero za wananchi

**Na Steven William,** MUHEZA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Tanga imesema hakuna kero ya mwananchi itakayokwama kutatua kwa sababu imejipanga kupita kwenye vitongoji, vijiji na kata kusikiliza na kuwaletea maendeleo.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) ya Muheza, Mohamed Mfaki, wakati akijibu kero za wananchi katika baadhi ya vijiji vya wilayani hapa.

Kwa mujibu wa Mfaki, Rais Samia Suluhu Hassan amewaagiza kuwatumikia wananchi, kutatua kero zao na kuahidi kufanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa.

" Kuna wananchi wanatoka kata za mbali na hawana uwezo wa kuja hapa halmashauri kuwasilisha kero zao, hivyo uongozi wa wilaya utakwenda katika kata na vijiji vyao kusikiliza na kutatua kero zao," alisisitiza Mfaki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Jumaa Mhina, alisema timu yake ya wataalamu imejipanga kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Baadhi ya wananchi waliofika kuwasilisha kero, wameupongeza uongozi wa wilaya hiyo kwa kuwasikiliza na kuahidi kutatua.

# Ajitolea kujenga ofisi za chama

**Na Steven William,** MUHEZA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Nkumba wilayani hapa, Mkoa wa Tanga, Hassan Mkebe, amejitolea kujenga ofisi mbili za chama hicho katika kata hiyo kwa gharama ya Shilingi milioni 22.

Mkebe aliyasema hayo wakati wa akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Kata ya Nkumba.

Alisema amejenga ofisi ya CCM ya tawi katika Kijiji cha Ubembe, ukumbi wa mikutano na vyumba vya maduka kwa gharama ya shilingi milioni 12.

Alisema baada ya kukamilika ujenzi wa ofisi hiyo, amejenga nyingine ya CCM ya Kata ya Nkumba kwa Shilingi Milioni 10. Mkebe, alisema pia amesaidia ujenzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo ya sekta ya afya, elimu na maji katika kata hiyo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Simon Leng'ese, katika sherehe za chama hicho kutimiza miaka 47 zilizofanyika katika kata hiyo, alimpongeza kwa kujenga ofisi hizo mbili za chama.

Aliwataka viongozi wengine wenye mapenzi mema kwa chama hicho kuiga mfano huo wa kukisaidia.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu, alimpongeza Mwenyekiti huyo kwa kujenga ofisi hizo akisema huo ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

Mwenyekiti wa CCM wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Aziza Mshakangoto na Jumuiya ya Wazazi, Hatibu Bakari, waliwataka wadau wa chama hicho kuunga mkono juhudi za mwenzao huyo wa Nkumba kwa kukipenda kutoka katika damu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kutoka chakacha hadi singeli

**Na Adam Fungamwango**

HIVI karibuni aliyekuwa msemaji wa klabu mbili kubwa nchini, Simba na Yanga, Haji Manara alisikika akisema yeye ni mkubwa sana hawezi kukaa na kuzungumza au kubishana na mtu anayeimba chakacha.

Ingawa hakumtaja, lakini kila mmoja hata mtoto mdogo anafahamu mkasa mzima wa Manara na Dulla Makabila. Wala sitaki kuingia sana ndani kwa hilo.

Baadhi ya waandishi wa habari waliposikia neno chakacha waliangua kicheko. Hata mimi niliposikia hivyo ikanikumbusha mbali sana.

Sasa leo hii nataka nielezee uhusiano au muingiliano wa muziki wa chakacha na singeli.

Dulla ni mwimbaji wa muziki wa singeli na siyo chakacha. Nadhani ilikuwa ni namna tu ya kuendelea kupigana vijembe. Lakini ukweli utabaki pale pale kuwa muziki wa singeli asili yake imetokana na chakacha, ingawa kwa sasa ni vitu viwili tofauti.

Kuna marekebisho na vionjo vingi vimeingizwa na kurekebishwa miaka ya sasa mpaka kutoka chakacha na kuipata singeli.

Mwandishi ameamua kuchimba huku na kule kuletea asili ya miziki hiyo, wanamuziki, bendi, nyimbo zake na jinsi ulivyokuwa ikibadilika kutokana na nyakati, vizazi, na mahitaji ya soko.

**CHAKACHA**

Chakacha ni muziki wa jadi na mtindo wa ngoma kwa waswahili wa pwani ya Kenya na Tanzania.

Awali ilikuwa inachezwa kwenye matayarisho ya harusi na kutazamwa na wanawake.

Baadaye muziki au ngoma hiyo ilianza kutazamwa na watu wa aina nyingine, lakini iliendelea kuwa na wapenzi wengi ambao ni kinadada na kinamama wa maeneo ya pwani.

Mwishoni mwa karne ya 20, vikundi na bendi za muziki zilichukua vionjo na kuviingiza kwenye vyombo vya kisasa, wakichanganya kidogo na staili ya Afropop.

Bendi za nchini Kenya kama Mombasa Roots, Safari Sound band na The Mushrooms ndiyo zilikuwa vinara kwa kupiga muziki huo na kufikia miaka ya 1970 mpaka mwanzoni mwa 1980 walitoa nyimbo nyingi za staili ya Chakacha.

Nyimbo hizo ni kama 'Disco Chakacha' mwenye maneno kama, 'bembea eee, bembea mtoto, leo ni leo tutauona mpambano kweli si uongo. Ana malele babu yao ana malele, ana mkia, lapaje, lapata hivi na unyandawe na mkono tele, ukabakia.' Huu ulikuwa wimbo maarufu zaidi wa chakacha eneo la Afrika Mashariki.



Kundi la Jagwa Music

Zingine ni 'Mwana Mbuzi Meme', 'Bonge Lote Nyama Mkononi', 'Watoto Nyara' na zingine nyingi.

**MCHIRIKU**

Baada ya kuonekana ni muziki wa akinamama zaidi, muziki huo uliboreshwa na baadhi ya wasanii na kuwekwa vionjo na kwa maajabu makubwa ukageuka na kuwa muziki uliopendwa zaidi na vijana wababe, wenyewe wakauita mchiriku.

Hapa ulibadilika na kinanda ndiyo kilishika hatamu zaidi na kuongoza muziki wenyewe.

Kwa bahati mbaya sana kutokana na mashabiki wake kuwa ni vijana wababe, watu wa rika lingine na wakiwemo wanawake hawakuupenda kwa madai ni muziki wa 'wahuni.'

Kulikuwa na ukweli ndani yake kwani sehemu ambapo siku hiyo muziki huo unapigwa laivu kwenye sherehe yoyote ya kijamii ni lazima kuwe na ulinzi mkali.

Hapo wakaibuka wasanii wengi waliouweka kwenye chati muziki huo kama Omari Omari, ambaye aliibuka na ngoma yake kali kipindi hicho mwishoni mwa miaka ya 1980 'Kupata ni Majaliwa.' Zingine ni 'Uchungu wa Mwana', 'Mfungwa Hachagui Gereza.'

Kundi la Atomic nalo lilitoa nyimbo zake kama 'Bwana Kipaka' na 'Tuache Tamaa.'

**MNANDA**

Mabadiliko ya muziki huo bado yanaendelea, kwani baada ya kinanda kuchukua nafasi kubwa zaidi, mwanzoni mwa miaka ya 1990, baadhi ya wasanii waliongeza na vionjo vya kuingiza ngoma zilizokuwa zikipigwa kama vanga ya Kizaramo, lakini kinanda bado kuhanikiza.

Mashabiki wa muziki huo wakabaki ni wale wale, waliitwa 'masela', jina la mchiriku likaondoka sasa ukaitwa mnanda.

Hapa yakaibuka makundi mapya yaliyoleta ushindani kama Gari Kubwa maarufu kama Meli ya Sumu ambao walitoa vibao vya kama 'Masuala ya Kubembea', 'Narudi Nyumbani', 'Ali Hassan Mwinyi', 'Sheli Mama', akaibuka msanii aliyeitwa Juma Mpogo, ambaye alikuja na nyimbo zake kama, 'Wametutoka', 'Lawama', 'Ajali ya Kibada' na nyingine nyingi.

Kundi la Jagwa nalo halikuwa nyuma, lilitoa albamu nyingi zikiwa na nyimbo kama 'Jenifer', 'Liwalo na Liwe', "Sarafina', 'Oscar Mkoba', 'Kuluthum', 'Mpangaji Mungu', na zingine kem kem.

Kwenye miaka ya 2000 kuliibuka baadhi ya wasanii wakali wengine wa mnanda ambao walikuja kisasa zaidi na kuongeza baadhi ya vionjo vya bongo fleva ndani yake.

Hao ni kama Dogo Mfaume na ngoma yake ya 'Kazi ya Dukani', Easy Man' naye akaja na kitu alichokiita 'Kasoro Wewe.'

**MDUARA**

Aina hii ya muziki ni mwendelezo ule ule wa kuanzia chakacha, mchiriku, na mnanda. Baada ya baadhi ya wanamuziki kuona umekuwa muziki wa wababe mno, walikaa chini na kuufanyia ubunifu zaidi.

Wengine waliona ni kama unaenda kupoteza uasili wake, hivyo wakarudi kwenye chakacha, wakaichukua ilivyo na kufanya ubunifu wao, wakaja na kitu kinachoitwa mduara.

Inafanana mno na chakacha, lakini muziki huu ukafanikiwa kuwateka hata wanaume ambao mwanzo hawakuwa wanacheza chakacha asilia.

Ni muziki uliokuja kuwakusanya watu wote, wanaume, wanawake, wazee, vijana, na hata mabosi wenye vyeo vya juu nao walikuwa wakijimwaga kucheza mduara.

Ulichezwa zaidi kwa watu kucheza wakiwa wamezunguka duara kiubavu na kwenda mbele huku wakicheza, wakizunguka, wakati mwingine kukatika na kushuka chini.

Bendi zilizotamba na aina hiyo ya muziki mwanzoni mwa miaka ya 2000 ni Chuchu Sound, waliokuwa vinara, Kilimanjaro Band 'Wana Njenje'.

Ni mtindo ambao ulitikisa mno kiasi kwamba hata baadhi ya bendi zingine kama TOT Plus nao wakaingia kwenye mkumbo huo.



Omari Omari mmoja wa waasisi wa Mchiriku

**SINGELI**

Wasanii wale wale wa mnanda nao wakajaribu kujiongeza. Kuanzia mwaka 2010, mnanda ukafanyiwa maboresho ukaingizwa vionjo vya taarab, bongo fleva, vanga na mdundiko wenye asili ya ngoma ya Kizaramo, kikazaliwa kitu kinaitwa singeli.

Wasanii waanzilishi ni kama Msaga Sumu ambaye aliibuka na ngoma ya 'Unanitega Shemeji.'

Ngoma hiyo iliteka hisia za mashabiki wengi na akatoa ngoma zingine, lakini pia akapata wapinzani ambao ni wasanii walioona inalipa nao wakaingia kwenye muziki huo akiwemo Dulla aliyetoa ngoma aliyoita 'Makabila', ambayo ndiyo iliyompa jina la Dulla Makabila.

**Tuma meseji 0716 350534**



Mduara

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Leonard Bandola, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa pikipiki za kubeba abiria maarufu bodaboda katika soko la vyakula la Michungwani, wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, akizungumza na masheikh, maimamu, walimu wa madrassa na wakuu wa idara, katika Msikiti wa Gadaf, jijini Dodoma juzi, wakati wa kikao cha kuwataka kuboresha miundombinu ya majengo ikiwamo madarasa na hosteli za wanafunzi. Wengine ni Mjumbe wa BAKWATA wa wilaya hiyo, Sheikh Ambar Mpenda (wa tatu kushoto) na (kulia) ni Katibu wa Baraza hilo wilaya, Ahemed Msuri. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Wakazi wa Kijiji cha Nyanguge, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, wakipata huduma ya maji katika moja ya mabomba ya majisafi na salama kutoka kwenye visima virefu vinavyotumia umeme kutoka kwa Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini (REA) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya. **PICHA: NDALIKE SONDA**



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Singida, Bertha Nakomolwa, akizungumza na wananchi wa Kata ya Ughandi, Halmashauri ya Wilaya ya Singida jana, wakati wa maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Polisi wa Kata ya Nambizo, wilayani Mbozi, mkoani Songwe, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Issa Mudu, akizungumza na mtoto wa Shule ya Msingi Utambalila, baada ya kuwapa elimu ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto, hivi karibuni. Aliwataka wanafunzi hao wasikae kimya wala kusita kutoa taarifa kwa jambo lolote ambalo watalitilia mashaka au la ukatili dhidi yao. **PICHA: POLISI SONGWE**



Mwendesha baiskeli ya magurdumu matatu maarufu kama guta, akiwa amebeba mzigo na abiria juu katika Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Usalama, Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**STEPHEN .W. MREMA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma vya kidato cha nne chenye index namba **S.2774-0199/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MSIMBAZI SECONDARY SCHOOL mwaka 2015 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0960-0882/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BENJAMIN WILLIAM MKAPA HIGH SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/13229/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHANGWE SAID KUNULILO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1197/0231** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia GREEN ACRES SEKONDARI mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/15044/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THE CATHOLIC DIOCESE OF IRINGA** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T 454 DMS** AINA YA LAND CRUISER HARDTOP RANGI NYEUPE ENGINE NO **1HZ0893289,** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA NAMBA: **PHQ/IRI/IRI1521/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE NO.24420D 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GRACE WILLIAM KILUA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY PETER EDWARD MLIMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 8th day of March 2024

**Dated at Korogwe this 8th day of February 2024**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE DISTRICT

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 155 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late HENRY PAULO KIMAMLE of Ihumwa Ward within Dodoma City Council**

**AND**

**In the matter of an application for Letters of administration by DONATUS PAUL KIMAMLE.**

**GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of 2..............2024. Dated at Dodoma this 29 Day of 12...............2023

.............................
**PETITIONER**

Presented for filing this 8.........day of 2..........................2024

.............................
RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:
PETITIONER
IHUMWA WARD
P.O.BOX 1249
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI
MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...7/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: ASHA ABDALLAH MGAGALA wa MAFIGA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOTOLEWA NA SIRI OMARI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi 2 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 6 mwezi 2 mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI
MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...6/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: TABIA MOHAMED wa MAFIGA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA BASHIRI MOHAMED**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 2 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 2 mwezi 2 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la madai/Ndoa Na. 07 ..................2024**

**Jina la Mdai NICKSON JACKSON KAWICHE**

**Jina la Mdaiwa TUMAINI LEMA NA AMANI URASA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA
(kanuni ya 18 ya kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa TUMAINI LEMA NA AMANI URASA
WA GOBA DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa Mdai/wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)
Ya pesa TSHS 2,380,000/= FIKA HAPA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KATIKA TAREHE PANGWA kwa hiyon unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 mwezi 02 Mwaka 2024 saa 2;30 Asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
Angalizo: kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurin. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi 02 Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO Enaboishu WILAYA YA Arumeru**

**SHAURI LA MADAI NA.101 YA 2023**

**Yogin Patel (Breakmass Lugendo) ......................... MDAI**

**Dhidi ya**

**Mathias Paul Mathias.........................................MDAIWA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)
(MCA Na. 2/1984)**

**Kwa Mathias Paul Mathias
Itigi Singida.**

Kwa kuwa umealazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka/ madai kuwa shahidi kama ifuatavyo.Fika mahakamani bila kukosa.
**UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya Jumatano tarehe 10/1/2024 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa .
**USIKOSE KUHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuachakuhudhuria mahakamani kosa k/f Na 114 A Sura 16 K/A. Hivyo Mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 19/12/2023.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
ENABOISHU

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MASIJALA NDOGO YA TEMEKE
(TEMEKE KITUO CHA JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 01 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**GEOFFREY HENRY ITEBA
NELLY GEOFFREY ITEBA.........................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa 02, 2024.

Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 08 mwezi wa 02, 2024

NAIBU MSAJILI

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

## MAMA MWENYE NYUMBA - 14

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Basi dada sasa hivi wanaishi Kinondoni Biafra."

"Wamepanga?"

"Wapange wapi? Wanakaa nyumba ya tajiri mmoja. Wao wameambiwa wailinde."

"Toba, ndiyo hivyo? Mbona nimeambia wamepanga nyumba nzuri tu, siyo kama kibanda chako, ina bomba, ila maji humo humo!"

"Wapi, wapi dada, habari zao zote ninazo, pesa ya kupanga chumba hawana, kuna mtu kawaonea huruma kaamua kuwaweka kwenye nyumba yake ili walinde."

"Hee makubwa."

"Mimi nililijua hili wakitoka kwangu hawawezi kupata sehemu kama yangu, bwana mwenyewe nasikia bodaboda yenyewe sasa hivi mbovu, pesa hana."

"Sasa Mwantumu maneno yote hayo yanakutoka, ulivyotaka kumpachika binti yako itakuwaje?"

Kitu ambacho hakukijua Bishada ni kwamba maneno yote aliyokuwa akiongea Mwantumu ni ya uongo.

Alikuwa akieleza maneno hayo kwa ajili ya chuki kwa sababu pamoja na yote yaliyotokea, bado Jonas amepatana na mkewe.

"Na nasikia juzi tu dada, mvua imenyesha maji hadi shingoni. Wamelala wima. Eneo hilo kumbe lina mafuriko, mbona kazi wanayo. Wamejifanya kuondoka kwangu hakuna lolote walilofanya. Wamekwenda kukaa nyumba ya bure kama wako bweni vile, na mafuriko juu."

"Isije tu ukawa unawasagia kunguni kumbe uongo!"

"Mtu aliyenipa data namwamini Bishada, na atahangaika sana kwa sababu baada ya hayo mafuriko kesho yake bwana kaenda kulala kwa ndugu zake, bibi huyo karudi huko huko kwa shangazi yake Kawe. Wanasubiri kukauke warudi tena hapo hapo. Wangebaki kwangu yote haya yangewapata kweli? Nyumba mbovu ndiyo lakini hakuna mafuriko."

******************************

Watu wanakwambia mtu atakunyima chakula lakini siyo maneno. Yote yakamfikia mwenyewe.

Kwanza kabisa yalimfikia Tabia, halafu yakamfikia Rozi.

Wote wakamtwangia simu rafiki yao na kumweleza maneno yote ya uongo yanayotolewa na mama mwenye nyumba dhidi yake.




**"Wewe, mimi nina ushahidi hadi sauti yako na video watu walikuwa wanakurekodi ulivyokuwa unaongopa."**

"Jamani huyu mama ananitakia nini mimi? Si nimehama kwake! Niko kwangu. Kwa nini aseme eti nimewekwa tu hapa ili tulinde? Nasema hivi. Mimi nakuja huko huko kesho kubwa!" Akasema Devota kwa hasira.

Alikuwa akiongea na Tabia kwenye simu. "Sikuliza Devota, wala usije kwanza. Wiki ijayo sisi tunahama hapa. Tumepata nyumba maeneo yale karibu na ulipomfumania mumeo shoga yangu wala siyo mbali, sasa wewe vumilia tukihama uje ili twende wote na sisi tuna hasira naye, sasa hivi bado tupo kwake hatutomfaidi." Akajibu Tabia akionekana kabisa na yeye amepania.

Rozi naye aliposikia hilo akamtwangia simu na kumuuliza msimamo wake baada ya uzushi huo.

"Nimeongea na Tabia, kaniambia eti mnahama wiki ijayo."

"Ndiyo shoga yangu tunahama tumwachie kijumba chake kibovu cha urithi."

"Nasikia mnahamia maeneo ambayo nilimfumania shemeji yako na Mwadawa."

"Enhee shoga, maeneo yale yale, nyumba kama ya nne hivi kutoka hapo, wote tumepata vyumba humo humo ndani."

"Hee hongereni Rozi mna bahati, mmekaa nyumba moja halafu mnahamia tena nyumba moja!"

"We acha tu shoga yangu. Si alihama mpangaji mmoja, halafu mwingine akawa amebakisha mwezi ahame, ikabidi tusubiriane."

"Sasa ni hivi, Rozi, mimi nataka nije huko niangushe varangati, naambiwa mimi eti namlindia nyumba tajiri wakati nimepanga nimetoa kodi ya mwaka mzima!"

"Njoo mwaya, yaani na sisi tulivyompangia huyu. Tunahama, halafu tunakusubiri ukija ukienda kumuuliza maswali na sisi tuko nyuma, ukilianzisha na sisi tumo, wala hatujali lolote tayari tumeshahama."

"Tabia kaniambia hivyo hivyo!"

"Basi ndiyo hivyo hivyo shoga yangu."

********************************************

"Enhe! Wewe aliyekwambia kuwa mimi pale tumewekwa tu na mume wangu tulinde nyumba ya tajiri hatuna uwezo wa kupanga ni nani?"

Ilikuwa ni sauti ya Devota. Sauti iliyoashiria shari na kuwa tayari kwa lolote. Kuna namna ambayo Mwantumu alikuwa jasiri kuwajibu utumbo Devota, Tabia na Rozi kwa sababu walikuwa ni wapangaji wake. Lakini sasa wameshahama wote.

Ilikuwa ni siku ambayo Devota aliisubiri kwa hamu. Yote aliyofanyiwa aliyeweka rohoni. Kusimangwa, kutishwa, kudhihakiwa, pamoja na aliyekuwa mama mwenye nyumba wake kutengeneza njama ya kumpa mumewe binti yake aliyaweka kwenye fundo moja.

Alikodisha bodaboda kutoka Kinondoni Biafra hadi Magomeni Mapipa kwa ajili ya kazi hiyo tu.

Wakati huo alikuwa akiwasiliana na shoga zake, Rozi na Tabia ambao nao walikuwa wamehama kiasi cha wiki moja iliyopita. Na hiyo ndiyo ilikuwa ni kampeni yao.

Akakaribishwa kwa wapangaji wenzake wa zamani. Wakapika chakula cha mchana wakala. Wakasubiri jua lipoe. Wakatimba nyumbani kwa mama Mwantumu wote watatu.

Wawili hawakuwa na kesi yoyote na mama mwenye nyumba wao wa zamani. Lakini moyoni walikuwa na visasi kwa jinsi walivyokuwa wakipelekwapelekwa.

Ila huyu mmoja alikuwa na kesi mkononi. Wakamkuta anaosha vyombo. Jinsi alivyowaona tu walivyokuwa wakija na kumsogelea alijua kuwa shari. Wote ni wapangaji wake ambao tayari wameshahama. Kwa nini waje tena pale? Na kwa nini waje wote?

Devota akarudia tena swali lile lile baada ya kuona hajibiwi. Safari hii akajibiwa.

"Siyo kweli, sijawahi kusema hivyo! Aliyekwambia ni mbea na mnafiki." Akajibu.

"Wewe, mimi nina ushahidi hadi sauti yako na video watu walikuwa wanakurekodi ulivyokuwa unaongopa."

Ni kweli. Watu walimrekodi Mwantumu.. Wengi walichoshwa na tabia yake ya ushakunaku, umbea na uzandiki. Kipande hicho wakamtumia mwenyewe.

Hakuwa mjinga kufunga safari kutoka Kinondoni hadi Magomeni kwa maneno matupu.

Akachukua simu yake na kubonyeza vitufe kadhaa ili kuifungua nywila, baadaye akafungua eneo la kuonyesha video na sauti.

Wakati huo tayari umati wa watu ulikuwa umeshajaa eneo hilo kama ilivyo kawaida tu ya uswazi. Watu wasisikie kitu.

Kila kitu kilisikika. Hata vile ambavyo hakuambiwa. Mwantumu aliona aibu na watu waliokuwa hapo wakaanza kumcheka, kumzodoa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PRISONS: KUCHEZA NA YANGA SI JAMBO JEPESI

**Na Oliver Albert**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Hamad Ally, amesema kucheza na Yanga si jambo jepesi lazima kujipanga, lakini wao wako tayari kuwakabili kesho.

Prisons itaikaribisha Yanga kesho kwenye uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ukiwa ni mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ally alisema Yanga ni timu kubwa yenye wachezaji wenye akili sana ya kutafuta matokeo hivyo lazima wawakabili kwa uangalifu.

"Maandalizi yetu kwa asilimia kubwa yanakwenda vizuri na tuko tayari kwa mchezo tukihitaji matokeo mazuri.

Yanga ina wachezaji wenye akili kubwa na jinsi unavyocheza nao lazima uwe makini sana kwa sababu inaweza kuamua matokeo kama timu muda wowote kwa mchezaji mmoja mmoja au mabadiliko ya mwalimu kwa wachezaji mechi inavyoendelea (sub).

"Kama timu pinzani mtakuwa na makosa ya kujirudiarudia muda wowote wanakuadhibu hivyo hata sisi tumekuwa na angalizo kwenye hilo," alisema Ally na kuongeza,

"Tunajua pamoja na ubora wao pia wana madhaifu ambayo ndio tunayafanyia kazi ili kujaribu kuona tunawazuiaje na tunapataje matokeo mazuri dhidi yao," alisema.

Aidha, kocha huyo alisema jambo la muhimu kwao ni kuhakikisha wanakuwa makini muda wote ndani ya mchezo ikiwa wana mpira au hawana.

Kocha Ally amekuwa na mwenendo mzuri tangu achukue mikoba ya kuinoa Tanzania Prisons Novemba mwaka jana. Katika michezo minne aliyoiongoza timu hiyo, ameshinda michezo mitatu na kutoka sare mchezo mmoja.




Msemaji wa kampeni ya magifti dabodabo, Haji Manara (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 30 mshindi Lillian Clement, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# *Lillian aibuka mshindi Shilingi mil. 30*

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Lillian Clement jana alitangazwa kuwa mshindi wa Sh. milioni 30 kwenye droo ya mwisho ya kampeni ya magifti dabodabo.

Mshindi huyo jana alitangazwa na kukabidhiwa mfano wa hundi ya fedha hizo na msemaji wa kampeni hiyo ya Tigo, Haji Manara, Mwananyamala jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi na kukabidhiwa zawadi yake, Lilian alisema anaishukuru Tigo kwa kumuwezesha kupata fedha hizo ambazo zitamsaidia sana.

Alisema hakuamini alipoambiwa ameshinda kiasi hicho cha pesa mpaka pale alipothibitishiwa na mfanyakazi wa kampuni hiyo na kuandaliwa tukio la kumtangaza.

"Pesa hizi zitanisaidia kwenye malengo yangu, nashukuru sana kwa kweli, nitaikumbuka siku zote kampeni hii na nitaendelea kuwa mteja wa Tigo," alisema Lillian.

Aidha, msemaji wa kampeni hiyo, Manara, alisema kampeni hiyo imefika ukingoni baada ya kuwapata washindi wa mwisho kwenye droo hiyo. "Lakini kumalizika kwa kampeni hii kunatoa fursa kwa kampeni nyingine kutoka tigo, Watanzania waendelee kutumia bidhaa za tigo na kushiriki kwenye kampeni zijazo ili waje kuwa kama Lilian, washinde pesa zitakazowasaidia katika mambo yao," alisema Manara.

## Namungo yazitaka pointi 9 ugenini

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mwinyi Zahera, ameanza kupigia mahesabu kuzipata pointi tisa kwenye michezo mitatu ijayo ya Ligi Kuu wakia ugenini wakianzia kesho Jumapili dhidi ya Tabora United.

Namungo watakuwa ugenini dhidi ya Tabora United kwenye Uwanja wa Alli Hassan Mwinyi mjini Tabora, baada ya hapo watashuka dimbani tena Februari 11 kucheza na JKT Tanzania kabla ya kucheza na KMC siku tano baadaye kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera alisema malengo yao kuvuna alama zote tisa katika michezo mitatu ya ugenini ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa ligi.

Alisema maandalizi yao yanaendelea vizuri na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya Tabora United ingawa wanatambua utakuwa mchezo wa ushindani.

"Tumejiandaa vizuri, wachezaji wote tuliokuja nao Tabora wako tayari kwa mchezo akiwamo mshambuliaji wetu mpya, Maddie Kagere ambaye ameungana na kikosi baada ya kumaliza changamoto za kifamilia kwao.

Malengo yetu ni kutafuta alama tatu katika kila mechi iliyopo mbele yetu tukianza na michezo mitatu ya ugenini tunahitaji kuvuna pointi zote na wala tusipoteze pointi," alisema Zahera.

Alisema wamefanyia kazi mapungufu yao hasa kwenye maeneo ya ulinzi na ushambuliaji na anaamini mambo yataenda vizuri kama anavyoyaona mazoezini.

## Uhamiaji FC yaitisha JKU Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Timu ya Uhamiaji FC, Abdul-Salehe Abdallah, amesema kuwa licha ubora wa vinara wa Ligi Kuu Visiwani hapa, JKU SC, matarajio yao ni kupata ushindi kwenye mchezo wao wa leo.

Timu hizo leo zinakutana kwenye Uwanja wa Mau A majira ya saa 10:00 jioni mchezo ambao unatarajiwa kuwa wenye upinzani mkubwa.

Uhamiaji FC inashuka uwanjani ikiwa na alama 19 na ipo nafasi ya tisa katika msimamo Ligi Kuu wakati wapinzani wao, JKU SC wakiwa na alama 39 wakiongoza kwenye msimamo.

Akizungumza na Nipashe jana, Abdallah alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa wanakutana na timu ambayo imeupania sana ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu.

Alisema katika mchezo huo atakuja na mbinu tofauti ili kuweza kupata alama tatu zitakazowafanya kutoka katika nafasi waliyopo na kupanda juu zaidi ili kuinusuru timu hiyo kushuka daraja.

Alisema kuelekea mchezo wao huo wamefanyia maboresho makosa yao waliyoyaona katika mchezo wao wa kwanza katika mzunguko huu wa pili ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huu wa leo.

"Mara nyingi makosa yetu ni yale yale yanajirudia ni suala la umakini kwa washambuliaji pale tunapopata nafasi lakini pia kuongeza umakini kwa walinzi pale ambapo sisi tunashambuliwa," alisema Abdallah.

Aidha, alisema katika mzunguko wa kwanza hawakufanikiwa kufanya vizuri katika hivyo mzunguko huu lazima wahakikishe timu inapata matokeo yatakayowafanya kusalia katika ligi hiyo msimu ujao.

Uhamiaji FC ndio timu inayoongoza kutoa sare nyingi katika michezo ya Ligi ambapo katika michezo 16 iliyocheza imepata sare michezo 10, imeshinda michezo mitatu na imefungwa michezo mitatu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**EVANS NA HATIMA YAKE**
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema hakuna uamuzi ambao umefanywa kuhusu hatima ya beki wa Ireland Kaskazini, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 36, au beki wa kati wa Ufaransa, Raphael Varane, 30. (***Express***)

**TONEY AFUATILIWA**
KLABU ya Manchester United inamfuatilia mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, lakini imesema ana thamani ya pauni milioni 70 hivyo basi haitajihusisha na ushindani wa kutaka kumsajili. (***Star***)

**MBAPPE KUTUA R' MADRID**
RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Javier Tebas amesema kuna uwezekano wa kati ya asilimia 55 hadi 60 Real Madrid kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25 kutoka Paris St-Germain msimu huu. (***Mirror***)

**ZUBIMENDI AWANIWA LIVER**
LIVERPOOL ipo tayari kutoa changamoto kwa Arsenal kwa ajili ya kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25 kutoka Real Sociedad. (***Football Transfers***)

**SALAH BADO AWINDWA SAUDIA**
KLABU ya Saudi Arabia, Al Ittihad itajaribu tena kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, msimu huu wa joto, baada ya kushindwa katika ombi la msimu uliopita. (***ESPN***)

**ARSENAL YAMGANDA WILLIAMS**
ARSENAL imekuwa ikimfuatilia winga wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21. (***Mirror***)

**PARTEY AFUATILIWA JUVE**
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Thomas Partey raia wa Ghana mwenye umri wa miaka 30 anaivutia klabu ya Juventus ya Italia. (Fichajes)

**DAVIES ANYATIWA**
REAL Madrid inamfuatilia beki wa kushoto wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester City na Liverpool. (***HITC***)

**ONANA ATAKIWA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United inamtaka kiungo wa kati wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 22. (***Football Insider***)

**LEWANDOWSKI KUMALIZIA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 35, ana mkataba na Barcelona ambao utaendelea hadi Juni 2026 na anataka kuutimiza. (***Sport***)

**ALCANTARA KUONDOKA**
LIVERPOOL haitarajii kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 32, kusalia katika klabu hiyo zaidi ya msimu ujao. (***Football Insider***)

**KIWIOR ATAKIWA MILAN**
KLABU ya AC Milan inatazamiwa kuwa miongoni mwa timu kadhaa za Italia kuonesha nia ya kumnunua beki wa Arsenal na Poland, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 23, msimu ujao. (***Evening Standard***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE: NAWEZA KUIACHA ENGLAND BAADA YA EURO 2024

**PARIS,** Ufaransa

**Kocha huyo amesema atafanya tathmini mustakabali wake baada ya michuano ya ....**

GARETH Southgate hajaondoa uwezekano wa kubakia kuwa kocha wa England hadi Kombe la Dunia la 2026, lakini amesema kwamba, atatathmini mustakabali wake baada ya michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2024, msimu huu wa joto.

Southgate, ambaye amekuwa akiinoa England tangu 2016, ana mkataba na Chama cha soka cha England, FA, hadi Desemba mwaka huu.

**"Kuna nafasi nzuri, nusu ya makocha hawatakuwa hapa baada ya Euro. Hilo ni soka la kimataifa," alisema Southgate baada ya droo ya Alhamisi ya Ligi ya Mataifa ya UEFA mjini Paris.**

"Lazima uone jinsi majira ya joto yanavyoenda, ni rahisi kama hivyo. Ninajua kile tunachoweza kufikia wakati wa majira ya joto, najua kiwango changu cha mafanikio, baada ya hapo ninatakiwa kufikiria kitu kingine chochote.

"Lazima tutoe onesho na lazima ufanye maamuzi bora kwa kila mtu. Sitakuwa katika nafasi ya kufanya uamuzi huo kabla ya mashindano."

Gareth mwenye umri wa miaka 53 ndiye kocha aliyefanikiwa zaidi England tangu Sir Alf Ramsey aliyeshinda Kombe la Dunia mwaka 1966, baada ya kuiongoza nchi yake hadi fainali ya Euro 2020 na nusu fainali ya Kombe la Dunia la 2018.

Hata hivyo, alifikiria kujiuzulu kufuatia England kufungwa na Ufaransa katika robo fainali ya Kombe la Dunia 2022 kabla ya kuamua kusalia kwenye usukani hadi euro 2024.

England ipo kundi moja na Slovenia, Denmark na Serbia katika Kundi C la Euro msimu huu wa joto.

Droo ya Ligi ya Mataifa ya Uefa Alhamisi iliiweka England katika kundi pamoja na Jamhuri ya Ireland, Finland na Ugiriki.



# NAHODHA NIGERIA ANALITAKA KOMBE LA AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

NAHODHA wa Nigeria, William Troost-Ekong amesema kunyanyua taji la Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, utakuwa wakati "wa kushangaza" kwake na kwa nchi yake.

Super Eagles waliiondosha Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti na kutinga fainali itakayopigwa Jumapili mjini Abidjan, ambapo watamenyana na wenyeji wa michuano hiyo, Ivory Coast.

Nigeria wamefika fainali yao ya kwanza tangu 2013, wakati walipotwaa taji hilo kwa mara ya tatu katika historia yao.

"Unaota wakati kama huo," beki huyo wa kati, Troost-Ekong alisema akiiambia BBC Sport Africa.

"Nimeiona mara nyingi sana. Na nimefumba macho. Kwa kweli kuwa huko Jumapili na kupata nafasi ya kufanya hivyo itakuwa hisia ya ajabu sana."

Nigeria hawakuwa miongoni mwa timu zilizokuwa zinapewa nafasi ya kutwaa taji hilo kabla ya fainali hizo, kutokana na uchezaji wao duni katika mechi zao mbili za kwanza za kufuzu kwa Kombe la Dunia la 2026 na nafasi yao ya kuwa timu ya sita-bora barani Afrika kulingana na viwango vya kimataifa vya Fifa.

Hata hivyo, Super Eagles imekuwa timu iliyoorodheshwa katika nafasi ya juu katika michuano hiyo tangu mwisho wa hatua ya 16 bora, ambapo mabingwa Senegal, Morocco na mabingwa mara saba Misri walitolewa.

Kocha wa Nigeria, Jose Peseiro amesema amekuwa na imani na timu yake, ambao walikuwa wafungaji bora wa kufuzu kwa fainali wakiwa na mabao 22.

"Niliposaini mkataba, nilisema nataka kushinda Afcon," alisema kocha huyo raia wa Ureno akiiambia BBC Sport Africa.

"Kwa vyovyote vile, sijui kama kila mtu aliamini au la. Nimeamini tangu dakika ya kwanza.

"Hatujashinda chochote hadi sasa - tunataka kushinda Afcon."

# Kessie: Ni miujiza kwa Ivory Coast

**ABIDJANI,** Ivory Coast

KIUNGO wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie amesema ni kama 'miujiza' wao kufuzu fainali ya kombe la mataifa ya Africa, AFCON.

Kessie aliibuka mchezaji bora wa mechi baada ya Ivory Coast kupata ushindi wa 1-0 kwenye nusu fainali dhidi ya DR Congo na sasa anaamini wanaweza kufikia kitu maalum katika ardhi ya nyumbani.

Kessie amekuwa mshiriki wa mbio za Tembo hao, akiendesha injini kwa nguvu na utulivu. Baada ya kupita katika kundi lao, Ivory Coast wameongeza matumaini ya ushindi wa 'muujiza'.

Naye nyota wa AC Milan, Kessie amedhamiria kutoa kwa mashabiki wa Ivory Coast.

"Unapokuwa na umati kama wetu, bora zaidi ulimwenguni, lazima tupite njia yote," alisema baada ya kuifunga DR Congo.

Ushindi huo ulifuatia hatua za uaminifu za Kessie kwenye chumba cha kubadilishia nguo wakati wa hatua ya makundi.

"Kufungwa na Equatorial Guinea ilikuwa ni mwamko kwetu. Tulichukua fursa hiyo kuzungumza kwa uaminifu na kuwajibika," alieleza Kessie.

Ivory Coast imezaliwa upya tangu wakati huo, na kuwa na kiwango cha kuvutia katika fainali hizi, hili ni muhimu zaidi.

Kessie anaamini fainali itakayofanyika katika uwanja wa Rais Alassane Ouattara inatoa motisha zaidi.

"Uwanja huu una jina la Rais wetu, na lazima tuuenzi. Bado tuna safari ndefu. Tunapaswa kuwa na historia iliyotukuka hapa, na ni juu yetu kuandika sura inayofuata," alisema.

Ushindi siku ya Jumapili utazua matukio ya kusisimua nchi nzima.

# Aubameyang awatajia Barca kocha mpya

**BARCELONA,** Hispania

PIERRE-Emerick Aubameyang amehimiza klabu yake ya zamani ya Barcelona kumteua Jurgen Klopp kama kocha wao mpya ajaye.

Miamba hao wa Katalunya watatafuta bosi mpya msimu wa joto kufuatia tangazo la hivi karibuni la Xavi kwamba atajiuzulu wadhifa wake.

Raia huyo wa Hispania alikuwa chini ya shinikizo kubwa katika wiki za hivi karibuni, huku kukiwa na matokeo mabaya, na alivijulisha vyombo vya habari kwamba mabadiliko yalihitajika miezi tisa tu baada ya kuiongoza klabu hiyo kunyakua taji la 27 la La Liga.

Klopp pia anaachana na vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool msimu huu wa joto, akitaja uchovu na kutoweza kufanya kazi hiyo "tena na tena na tena", na akapendekeza kwamba huenda asichukue jukumu lingine katika usimamizi.

Licha ya maneno hayo, kocha huyo mwenye umri wa miaka 56 amekuwa akihusishwa sana na kibarua cha timu ya taifa ya Ujerumani, na pia amekuwa akitajwa kuwa mrithi wa Thomas Tuchel katika klabu ya Bayern Munich, iwapo miamba hao wa Bavaria watashindwa kuwashinda Bayer Leverkusen katika ubingwa wa Bundesliga.

Lakini Aubameyang, ambaye sasa anaichezea Marseille ya Ufaransa anapoelekea mwisho wa maisha yake ya soka, anaamini Barcelona wanapaswa kumfuata Klopp mara tu atakapoondoka Anfield, baada ya kucheza chini yake kule Borussia Dortmund.

"Klopp anakupa kila kitu, nguvu, ameshinda mataji makubwa, ni kocha mzuri," alisema akimwambia mwandishi wa habari, Gerard Romero wa chaneli ya Twitch.

"Ikiwa kuna nafasi kwa Barca ni chaguo zuri.

"Nilistarehe sana nikiwa naye Dortmund. Litakuwa jambo zuri kama anaweza kwenda Barcelona."

Uchezaji wa Aubameyang akiwa Barcelona ulikuwa mfupi na mtamu, ulidumu kwa miezi saba tu, lakini alifanya vyema kwenye LaLiga.

Baada ya kuwasili kwa uhamisho wa bure - aliondoka Arsenal kwa hasira baada ya kuvuliwa unahodha wa klabu na kocha Mikel Arteta, na sasa kiwa na umri wa miaka 34 amefunga mabao 11 katika mechi 18 za LaLiga, hasa akifunga mabao mawili katika mechi ya kukumbukwa ya ushindi wa 4-0 ugenini dhidi ya wapinzani wao Real Madrid.



## HABARI MICHEZO

# YANGA YAPELEKWA POLISI, SIMBA TRA

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) jana limetoa ratiba ya raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho (FA) ambapo vigogo wa soka, Simba na Yanga zimepewa 'mchekea'.

Mabingwa watetezi wa kombe hilo, Yanga wenyewe wamepangiwa kucheza na Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Februari 20 kwenye Uwanja wa Azam Complex wakati Simba watacheza timu ya daraja la pili ya TRA Februari 27 kwenye uwanja utakaotangazwa baadaye.

Kwa mujibu wa ratiba ya hiyo, Azam FC yenyewe ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani itaumana na Green Warrior Februari 22.

Ratiba hiyo inaonyesha kuwa Coastal Union itacheza dhidi ya Mbeya Kwanza Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Februari 19, Singida Fountain Gate itakipiga dhidi ya FGA Taletns, Uwanja wa CCM Kirumba siku hiyo hiyo huku Dodoma Jiji ikicheza na Biashara United kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma wakati Rhino Ranger itakipiga na Mbao FC kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Februari 20, Mashujaa FC itakuwa Lake Tanganyika Kigoma kucheza dhidi ya Mkwajuni, KMC itacheza dhidi ya Gunners FC wakati Kagera Sugar itakuwa Kaitaba, Bukoba kucheza dhidi ya Pamba FC.

Mechi za Februari 21 zitahusisha Tabora United itakayoumana na Stand United wakati Namungo ikiwa nyumbani itacheza na Transit Camp.

Siku moja baadaye Ihefu itacheza na Mbuni FC, JKT Tanzania itaumana na TMA Stars wakati Geita Gold itacheza dhidi ya Mbeya City.




Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Said (katikati), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (kulia), wakati wa uzinduzi wa ofisi mpya za klabu hiyo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Gamondi awakingia kifua wachezaji*

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amewakingia kifua wachezaji wake wapya na kuomba wapewe muda ili waonyeshe uwezo wao.

Kauli hiyo ya Gamondi imekuja baada ya baadhi ya mashabiki wa timu hiyo kuonyesha kutoridhishwa na baadhi ya wachezaji wao wapya akiwamo mshambuliaji Joseph Guede ambaye katika mechi mbili za Ligi Kuu alizocheza bado hajaonyesha makali yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi alisema wachezaji hao wapya wanahitaji kupewa muda zaidi ili waweze kuzoea mazingira ya Tanzania na uchezaji wa timu yao.

"Ni wachezaji wazuri, bado mapema sana kuanza kuhoji uwezo wao, ningependa wapewe muda zaidi waonyeshe makali yao, wanahitaji kuzoeana na wachezaji wenzao waliowakuta lakini wazoee ligi," alisema Gamondi.

Akizungumzia mchezo wao uliopita dhidi ya Mashujaa ambao walishinda kwa mabao 2-1, Gamondi alikiri mchezo huo ulikuwa mgumu na iliwalazimu kutumia akili za ziada kuweza kushinda.

"Tulikuwa na mchezo mzuri muda wote tulikuwa tunashambulia na mfano kipindi cha kwanza kulikuwa na uwezekano wa kupata penalti mbili kwa makosa waliyofanya wapinzani lakini waamuzi hawakutupa, hata hivyo mchezo ulikuwa mgumu kutokana na namna wapinzani wetu walivyokuja," alisema Gamondi.

Pia kocha huyo alikiri kuwa na mapungufu kwenye safu yake ya ushambuliaji lakini anaendelea kulifanyia kazi huku akitaka safu yake ya ulinzi kuwa makini zaidi.

"Kwa sasa kikubwa mpira kuingia nyavuni, umeona Mudathir ameweza kufunga bao la pili na kutupatia ushindi na kuondoka na pointi, tunarudi uwanja wa mazoezi kwa ajili ya mchezo ujao," alisema Gamondi.

Kuhusu kuwatoa Khalid Aucho na Pacome Zouzoua kwenye mchezo huo, Gamondi, alisema walionekana kuumia na kumlazimu kuwatoa kwa kuhofia kuwakosa kwenye michezo mingine ya mbele ambayo ni mingumu zaidi.

Yanga inatarajiwa kucheza na Tanzania Prisons kwenye mchezo wa Ligi Februari 11 na baadaye kucheza mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad.

## Waibuka washindi simu janja droo AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya washindi wanne wametangazwa jana kujishindia simu janja kwenye droo ya tatu ya AFCON ushindi ni Sportpesa iliyochezeshwa jijini Dar es Salaam.

Droo hiyo sehemu ya promosheni iliyoandaliwa na SportPesa katika msimu huu wa AFCON na pia ni mwendelezo wa zawadi ambazo zinatolewa kila siku.

Akizungumza baada ya droo iliyochezeshwa Makao Makuu ya SportPesa, Ofisa wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Lydia Solomon, alisema droo hiyo ni mwendelezo wa msimu huu wa fainali za AFCON.

"Kama mnavyofahamu leo (jana) imechezeshwa droo yetu ya tatu ya AFCON, Ushindi ni SportPesa ambapo wateja wanne kutoka Moshi, Dodoma na Dar es Salaam, wameshinda simu janja, baada ya kubashiri na kuibuka washindi, tunaendelea kuwahimiza wateja wetu kuendelea kucheza na SportPesa ili waweze kujishindia zawadi hizi kwenye msimu huu," alisema Lydia.

Aidha, aliwataja washindi hao wa nne kuwa ni Issa Ali kutoka Dodoma, Elia Massawe kutoka Moshi, Kilimanjaro, Lawi Mkwawa na Imaya Ramadhani wa Dar es Salaam.

Alisema kampeni hiyo inalenga kuwazawadia wateja wote wa SportPesa kupitia mitandao yote ya simu.

# Chama aiokoa Simba, Dube bado mwiba

INATOKA UK 24

hiyo iliyomkuta mfungaji akiwa katikati ya mabeki wa Simba na kuunganisha moja kwa moja nyavuni baada ya kuwazidi ujanja mabeki wa Simba.

Sare hiyo inazifanya timu hizo kugawana pointi moja moja, zikibaki kama zilivyo katika msimamo wa ligi, Azam ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi zake 32 na Simba katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 30.

Hata hivyo, Simba ina mchezo mmoja mkononi, ikicheza mechi 13, wakati Azam ikiwa imefikisha jumla ya mechi 14 sawa na Yanga.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kushusha presha ambapo sasa inakuwa imeizidi Simba kwa pointi saba ingawa Simba ina mchezo mmoja mkononi na imeizidi Azam kwa pointi tano huku wakiwa wamelingana idadi ya michezo waliyocheza.

# Michezo
Nipashe

Jumamosi Februari 10, 2024





Nahodha Nigeria analitaka kombe AFCON UK. 22




Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (kushoto), akimtoka beki wa Simba, Shomari Kapombe, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa jana Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. Timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: BINZUBERY**

## Chama aiokoa Simba, Dube bado mwiba

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Clatous Chama dakika za majeruhi jana liliiokoa Simba na kichapo kutoka kwa Azam FC katika mchezo uliochezwa CCM Kirumba Mwanza na timu hizo kufungana bao 1-1.

Chama alifunga kwa mkwaju wa faulo ya moja kwa moja baada ya mshambuliaji aliyeingia kipindi cha pili, Pa Omari Jobe kuangushwa pembeni kidogo ya eneo la hatari na Mzambia huyo kupiga kwa ufundi mpira wa huo wa faulo ulioenda moja kwa moja nyavuni na kumshinda kipa wa Azam, Mohamed Mustafa.

Kabla ya bao hilo, Simba ilikuwa nyuma kwa bao la kutangulia lililofungwa dakika ya 13 na mshambuliaji Prince Dube ambaye katika mechi za misimu ya karibuni amekuwa na kawaida ya kuifunga Simba.

Mzimbabwe huyo alipachika bao hilo baada ya kuunganisha krosi kutoka wingi ya kushoto iliyopigwa na Pachal Msindo.

Mpira ulianzia nyuma kwa mabeki ambapo Yannick Bangala alipiga pasi ndefu kwa Msindo, akamuacha Israel Mwenda na kukokota mpira kwa umbali mrefu kabla ya kupiga krosi

INAENDELEA UK 23

# Tanzania mwenyeji CHAN 2024

## Waziri Ndumbaro athibitisha bungeni, viwanja viwili kutumika, TFF yanena...

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA rasmi imeteuliwa kuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika Septemba mwaka huu.

Akithibitisha hilo bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amesema Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), limeiteua Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda kuwa wenyeji wa michuano hiyo.

Dk. Ndumbaro amesema nchi hizo zimepewa uwenyeji huo ili iwe kama maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON za mwaka 2027 ambapo nchi hizo za Afrika Mashariki zitakuwa wenyeji.

"Tanzania, Kenya na Uganda tutakuwa wenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika 2027, sisi tunaiita 'Pamoja AFCON' kwa sababu ni mara ya kwanza katika historia ya Bara la Afrika nchi zaidi ya moja zinaandaa mashindano kama haya.

> **Lakini kabla ya Pamoja AFCON, mwaka huu Septemba nchi hizi tatu zitakuwa wenyeji wa pamoja wa mashinda no ya CHAN, mashinda no haya ni kwa ajili ya wachezaji wanaocheza Iza ndani," alisema Ndumbaro na kuongeza;**

"Sisi Watanzania tutakuwa na vituo viwili, Dar es Salaam na Zanzibar, Kenya na Uganda pia watakuwa na vituo viwili viwili," alisema waziri huyo.

Alisema viwanja vitakavyotumika kwenye fainali hizo kwa upande wa Tanzania ni Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Uwanja wa New Amani Complex, Zanzibar.

Fainali zilizopita zilichezwa nchini Algeria ambapo timu ya Taifa ya Senegal ilitwaa ubingwa kwa kuwafunga wenyeji kwa mikwaju ya penalti 5-4, baada ya kutoka suluhu dakika 120.

Akizungumzia AFCON 2027, Waziri Ndumbaro alisema Tanzania itatumia viwanja vitatu na kuwatoa hofu wabunge na Watanzania kuwa kila kitu kitakuwa tayari ndani ya muda.

"Sasa nikiongelea AFCON ya 2027, Tanzania itatumia viwanja vitatu, cha kwanza ni cha Benjamin Mkapa ambacho kitakuwa tayari Agosti mwaka huu, Uwanja wa Amaan Zanzibar uliofanyiwa maboresho makubwa na kuzinduliwa Desemba mwaka jana, kwa maana hiyo uko tayari, uwanja wa tatu ni wa Arusha ambao tunategemea ndani ya mwezi huu wa pili, mkandarasi atakabidhiwa eneo ili kuanza ujenzi," alisema Ndumbaro na kuongeza;

"Nimeyasema haya ili kuwatoa hofu wabunge na Watanzania wote, viwanja viwili tayari vipo na wa tatu tutaumaliza kujenga kwa wakati kule Arusha," alisema waziri huyo.

Kwa upande wa TFF, Msemaji wa Shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, alisema suala hilo la kuwa mwenyeji wa CHAN liligusiwa siku za nyuma na Rais wa Shirikisho hilo, Walance Karia na sasa ni rasmi CAF wamewapa uwenyeji.

"Maandalizi yote ya CHAN na AFCON yameshaanza na yanaendelea vizuri," alisema Ndimbo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >